Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 8 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake Bungeni:-

Mheshimiwa Danhi Beatus Makanga.

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninazo taarifa mbili kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Taarifa ya kwanza ni kuhusu Miswada iliyopitishwa na Bunge hili katika Mkutano wake uliopita ilikuwa ni Miswada sita, taarifa ni kwamba yote imeshapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Taarifa ya pili, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba katika Mkutano uliopita tulipitisha Azimio la kumpa pole Mheshimiwa Rais kwa sababu ya janga la moto lililotokea nyumbani kwake. Mheshimiwa Rais alipokea ujumbe mlionituma kumpelekea na aliandika barua ya majibu inayosomeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Pius Msekwa, Spika wa Bunge la Tanzania, Dodoma. Shukrani.

Mheshimiwa Spika, nimepokea kwa shukrani kubwa barua yako ya tarehe 21 Aprili, 2004 iliyoniletea Azimio la Bunge Namba 28 la mwaka 2004 kuhusu tukio la moto uliounguza jengo la makazi ya Rais.

Sasa ninaandika kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa upendo wenu kwangu na kwa salaam za pole mlizonitumia. Kwa niaba ya mama Mkapa na familia yangu ninawashukuruni sana. Nazidi kukutakieni kazi njema. Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):-**

Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Takwimu za Chakula Kilichopelekwa Wilayani

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa baa la njaa limewasumbua wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu; na kwa kuwa hadi sasa hakuna takwimu sahihi za chakula kinachopelekwa kwenye kila Wilaya na fedha za usambazaji wa chakula hicho hadi vijijini:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa takwimu sahihi za kiasi cha chakula kilichopelekwa kila Wilaya hadi kufikia Machi, 2004 pamoja na fedha zilizotumika kusafirishia chakula hicho kwenye Wilaya na Taarifa hizo zitolewe kwa kila Mbunge?

(b) Kama takwimu katika sehemu ya (a) ya swali hili zikitofautiana na hali halisi iliyojitokeza Wilayani; je, Serikali itatoa tamko gani juu ya kasoro hizo?

(c) Kwa kuwa katika maeneo ya Kidugalo, Mkulazi, Tununguo, Mikese, Ngerengere na kijiji cha Mkambalani, kwa asilimia kubwa walitangaziwa kuwa chakula kililetwa na Kanisa; jambo nililolikanusha, je, Serikali itakuwa tayari kuchunguza na kumpata mtu aliyelipakazia Kanisa, na kumchukulia hatua za kinidhamu kwa kitendo cha kugushi mali kauli na kutumia nguvu za Serikali kinyume na maadili ya Kanisa?

Naomba swali namba moja la leo lijibiwe lakini kifungu cha (a) walete kwa maandishi.

**SPIKA:** Masharti hayakubaliwi swali litajibiwa kwa mdomo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Kisange Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwanza kama alivyoanza mwenyewe kwenye utangulizi wa swali hili lililoandikwa, naomba kukanusha kwamba Serikali hadi sasa haina takwimu sahihi za chakula kilichopelekwa Wilayani na fedha za kusambazia, takwimu zipo na zimekuwa zikitolewa kila mara katika Bunge hili na leo pia kama alivyoomba mwenyewe nitampatia. Tulishawahi kutoa vitabu kama hivi hapa ambavyo vina takwimu zote zinazohusika.

(a) Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa katika kipindi cha mwezi Juni na Julai, 2003, ilionyesha kuwa watu wapatao milioni mbili watakuwa na upungufu wa chakula ifikapo Oktoba/Novemba, 2003 na watahitaji chakula cha msaada kilichokadiriwa kufikia tani 77,490 za nafaka hususan mahindi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 25 Mei, 2004 Serikali ilikwisha kugawa tani 30,370 za mahindi. Mahindi haya yameuzwa kwa shilingi hamsini kwa kilo kwa kila mlengwa. Utaratibu huu ulizingatia mwongozo wa kuhakikisha chakula kinapatikana na kuwafikia wananchi wengi. Aidha, jumla ya shilingi 1,147,999,500/= zimetumika kusafirisha chakula hicho kutoka Vituo vya Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* vilivyo karibu hadi Makao Makuu ya Wilaya. Wilaya 70 ndizo zilizokuwa na upungufu wa chakula na kupelekewa chakula hicho.

Serikali pia ilipata chakula cha msaada kupitia Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* jumla ya tani 29,068 ambazo zimegawiwa bila malipo yaani bure kwa kutumia Asasi mbalimbali ambazo orodha ninayo na nitampatia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kusambaza chakula cha msaada kama nilivyoeleza, ilisimamiwa na Uongozi wa Mikoa na Wilaya kwa makini sana. Viwango vinavyotolewa na *SGR* vilihakikiwa na wahusika walikiri ni sahihi kama kutakuwepo na kasoro ambazo zitajitokeza katika utekelezaji zitatatuliwa kufuatana na taratibu zilizopo za kushughulikia matatizo yanayojitokeza katika utendaji wa Serikali.

(c) Mheshimiwa Spika, ugawaji wa chakula cha msaada katika maeneo aliyotaja Mheshimiwa Mbunge na pia katika Wilaya ya Morogoro Mjini ulisimamiwa vizuri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Chakula

kilipelekwa kwenye Kata zote zilizotajwa. Taarifa ya Mkoa wa Morogoro iliyonifikia tarehe 28 Mei, 2004, inaonyesha mgao wa chakula cha msaada kutoka Serikalini kwa Tarafa ya Ngerengere, Kata ya Ngerengere, Mkulazi, Kidugalo na Tununguo na Kata za Mikese na Mkambalani. Orodha ninayo na Mheshimiwa Mbunge nitakupatia.

Aidha, kiasi cha tani 20 za mbegu za mahindi zilizotolewa na Serikali katika maeneo hayo. Hii ilikuwa jitihada za Serikali katika kukabiliana na tatizo la njaa kwa kuwezesha maandalizi katika kilimo na zilipitia katika Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* na zilisambazwa na Shirika la *CARITAS.* Huo ndio utaratibu uliotumika na sio sahihi kwamba misaada hii ilitolewa na Kanisa. Hivyo, maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ilibidi alikanushe jambo hilo ni sahihi kabisa.Ingawa ni kweli pia madhehebu ya dini yametoa chakula cha msaada katika maeneo mbalimbali nchini lakini siyo katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa kushirikiana na viongozi ambao ndio wawakilishi halali wa wananchi na pale watakapojitokeza watu au mtu kupotosha azma hiyo kwa sababu yoyote ile hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake. Pale ambapo taasisi kama vile Kanisa itajitokeza kusaidia tatizo linaloikabili jamii, Serikali haitasita kushirikiana nao.

Mwisho, napenda kuwashukuru wale wote waliotoa misaada ya chakula na nchi marafiki waliotoa fedha za kununuliwa chakula na mbegu, viongozi wa Mikoa na Wilaya kwa usimamizi mzuri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ufuatiliaji.

**MHE. SEMIND K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani kwa Serikali kuleta vyakula hivyo na usambazaji. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Jibu sahihi limeonekana kwenye takwimu, lakini alipojibu swali langu mwezi wa juzi katika Bunge lililopita alisema kuna vyakula vya bure kwa ajili ya wazee na walemavu, kuna chakula cha kazi na chakula cha kuuza kwa bei nafuu. Sasa kwa taarifa tu vijiji 18 ambavyo *sample* ninayo hapa wameuziwa chakula hicho hakuna cha bure hata kimoja katika vijiji 18 vya tarafa ya Ngerengere vimeuzwa kwa bei nafuu. Matokeo matajiri waliwapa fedha watu wakanunua ili wawepe kidogo kwa utaratibu huo.

Je, anaweza akafuatilia hilo au kuundwe Tume Maalum ya kufuatilia hilo katika Mikoa ya Singida, Dodoma na Morogoro?

(b) Kwa kuwa wasafirishaji walikuwa *CARITAS* kupeleka hadi nimesema jibu langu vijijini, lakini vijiji vya Mkulazi kama nilivyosema kilometa 70 na kijiji cha Kisemu na kijiji cha Seregetebaa walifuata chakula hicho katika Makao Makuu ya Tarafa ya Ngerengere kilometa 70, kwa hiyo, matokeo wengine hawakukipata. Je, inawezekana akawa ameandikiwa taarifa ambazo si sahihi anaweza akafuatilia hilo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, misaada ya Serikali imetolewa ya aina tatu.

Kwanza ni chakula kilichotolewa na Serikali ambapo Serikali ilitenga tani 32,000 kwa ajili ya kuwapa wananchi walioathirika kutokana na takwimu zilizokuwepo. Huo ulikuwa ni mkakati ambao tulikubaliana na wadau wenzetu. Kwa sababu sisi ni *signatory* wa Mashirika yote yanayohusiana na maafa katika dunia hii. Wenzetu walisema watatusaidia tani 44,000 sisi tukasema tutachangia tani 32,000 na ndiyo maana mpaka sasa zilizochukuliwa ni tani 30,000 kati ya mgao ambao Serikali iliji-*commit* tani 32,000 na wenzetu hao wahisani wameishatoa hizo tani 29,000.

Kwa hiyo, sisi tulitoa chakula tukauza shilingi 50,000 lakini wale wadau walitoa chakula cha bure. Lakini kama Mbunge alivyosikia takwimu zangu waliahidi tani 44,000 zikapatikana tani 29,000, kwa hiyo, isingewezekana Mikoa yote wakapata chakula cha bure. Wilaya ya Morogoro na Mkoa wa Morogoro walipata kile chakula cha bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo, hawakupata chakula cha bure.

Takwimu na maelezo yote yanatolewa kutoka kwenye taarifa nitakayokugawia leo ambayo inaonyesha ni Mikoa gani wamepata chakula cha bure na Mikoa gani wamepata chakula cha bei nafuu na Mikoa gani walipewa mahindi kupitia kwa wafanyabiashara ili wanunue kutoka *SGR* kwa bei nafuu yaweze kuuzwa kwa wananchi kwa bei nafuu ili kushusha bei au ongezeko la bei kubwa katika Mikoa hiyo. Kwa hiyo, hizi ndiyo aina tatu za chakula kilichokuwepo.

Hili lingine alilouliza la pili, itabidi nifanye utafiti, kwa sababu sisi tulikuwa tunatoa mgao kwa Wilaya. Tunatoa mgao kwa kila Wilaya tunawapa na fedha, Wilaya ya Morogoro tuliwapa milioni 15 kwa hizi za Serikali maana hizo za bure hazikwenda. Wao ndiyo waliokuwa wanafanya utaratibu wa kuchukua wala si kupitia *CARITAS.* Hiki chakula cha bei nafuu kilichukuliwa kwa usimamizi wa Serikali katika nchi nzima. Sasa kama hakikufika au ilikuwaje tutafanya utafiti ili tuone ilitokea namna gani.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kuna sehemu ambazo zimekabiliwa na ukame tena mwaka huu, hasa Arusha na Kilimanjaro nimepita huko. Je, Serikali imeweka mikakati gani mwaka huu ya kuhakikisha kwamba wananchi wa sehemu hizo ambazo zimepata ukame wanapewa chakula cha kutosha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo habari kwamba baadhi ya maeneo mvua bado zimekuwa haba mwaka huu, lakini Serikali imeamua kufanya tena tathmini nyingine ili kujiridhisha vizuri zaidi kitaalamu na iweze kupata hasa hasa tathmini ambayo itaiwezesha Serikali kujiandaa vizuri kukabiliana na maafa yoyote yatakayojitokeza.

Kwa hiyo, tathmini hiyo haijafanywa, lakini hivi sasa Serikali inajiandaa kufanya tathmini tena nchi nzima ili kuweza kujua ni misaada gani itatakiwa na aina gani ya maafa yatakayojitokeza katika maeneo ambayo mvua hazikunyesha vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na swali linalofuata, napenda kuwatambulisha wageni wa Kimataifa walioko katika *Gallery* ya Bunge leo. Tunao ujumbe wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Kenya ambao wanatutembelea hapa Dodoma leo na kesho na hivi sasa wako katika *Gallery* ya Bunge wanasikiliza kipindi cha Maswali na Majibu. Nitawaomba wasimame ili tuweze kuwapokea. Wamefuatana na Balozi wa Kenya nchini Tanzania. *(Makofi)*

Na. 2

## *Facilities* za Michezo kwa Waheshimiwa Wabunge

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA (k.n.y MHE. MWADINI ABBAS JECHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa imekuwa ni jambo la kawaida kwa Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa kwenye Mikutano yake ya Bunge Dodoma hujishughulisha na michezo; na kwa kuwa Ofisi ya Bunge mpaka sasa haijajenga viwanja na majengo yake binafsi ya michezo, jambo ambalo linarejesha nyuma ari ya kushiriki michezo mbalimbali hasa *indoor games,* na kwa kuwa ujenzi wa ukumbi mpya wa Mikutano ya Bunge haukushirikisha ujenzi wa majengo ya michezo ya ndani ambayo ingewapa fursa Waheshimiwa Wabunge kushiriki vyema katika michezo hiyo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujenga viwanja na majengo yatakayowekwa vifaa kamili na walimu ili Waheshimiwa Wabunge wapate fursa nzuri zaidi ya kushiriki michezo hiyo?

(b) Kama umuhimu huo upo; je, ni lini Serikali inatarajiwa kujenga viwanja na nyumba za michezo ili kukidhi haja inayokusudiwa?

(c) Je, Serikali iko tayari kuandaa ziara ya kimichezo kwa timu za michezo mbalimbali za Bunge ndani na nje ya nchi ili kukuza mahusiano ya kimichezo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Utaani, naomba kutoa maelezo machache ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Tume ya Huduma za Bunge kwa kutambua umuhimu wa kuboresha afya za Waheshimiwa Wabunge ilifanya mchakato wa namna ya kuboresha na kukidhi mahitaji ya Waheshimiwa Wabunge.

Katika mchakato huu, uliotokana na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano *(Five Year Development Plan)* Ofisi ya Bunge imepewa idhini na Tume kuendelea na utekelezaji kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mbunge wa Utaani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tume ya Huduma za Bunge yenye mamlaka ya kusimamia shughuli za Bunge ilikwisharidhia ujenzi wa jengo la kisasa litakalokidhi mahitaji ya michezo na mazoezi ya viungo *(Sports and Fitness Center).*

(b) Kwa kuzingatia ridhaa ya Tume, Serikali ilimilikisha Ofisi ya Bunge jengo la Kampuni ya Magari Tanzania yaani *Tanzania Motors Services Co. Ltd.* ili lifanyiwe ukarabati na litumike kwa ajili ya mahitaji husika. Makabidhiano ya jengo hilo hayajafanyika, yatafanywa baada ya taratibu fulani kukamilika. Kwa sasa Waheshimiwa Wabunge wameendelea kutumia viwanja vya michezo vilivyopo hapa Dodoma na huduma mbalimbali ambazo sasa zimejitokeza zimewekwa katika mji huu wa Dodoma katika hoteli mbalimbali hasa *Dodoma Hotel.*

(c) Pamoja na mahitaji hayo ya majengo ya michezo, Ofisi ya Bunge imekuwa na utaratibu wa kuandaa ratiba na ziara za michezo ya Kibunge kwa kuzingatia uwezo wa kifedha na nafasi ya Waheshimiwa Wabunge na imekuwa ikishirikisha timu zote za michezo ya mpira wa miguu na mpira wa mkono.

Naipongeza sana Kamati ya Michezo ya Waheshimiwa Wabunge chini ya uongozi wa Mheshimiwa Joel Bendera ambao umekuwa ukijitolea muda mwingi kufanikisha masuala ya michezo kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kutekeleza azma hiyo ili mpango huu ukamilike kama ulivyopangwa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja tu la kumuuliza.

Kwa kuwa sasa tupo katika kuimarisha uhusiano wa Afrika Mashariki; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge hili kuwa Serikali iko mbioni kufanikisha mpango huu wa michezo. Je, haoni sasa ni wakati maridhawa ili kuiandaa timu yetu katika mwaka huu kuipeleka katika moja ya nchi mbili ama Kenya au Uganda kwa ajili ya shughuli hizo za michezo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa katika ratiba ambazo zinapangwa na Kamati inayohusika na michezo ya Bunge

tumekuwa tunafanya michezo na mashindano mbalimbali na majirani na wenzetu ambao ni wanachama wenzetu wa Afrika Mashariki na leo mashahidi wako hapa na mara nyingi tumekuwa tunawafunga vile vile.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi hilo nitalifikisha kwenye Kamati inayohusika na michezo kwa kuzingatia Bajeti ambayo mtaiona ambapo Ofisi ya Spika wameweka bajeti maalum mahususi kwa ajili ya shughuli za michezo, lakini ratiba tuitafanya kwa ushirikiano na Uongozi wa Kamati ya Michezo ya Waheshimiwa Wabunge yenyewe.

Na. 3

**Mkataba wa *East African Customs Union***

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI (k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imeingia kwenye Mkataba wa *East African Customs* yaani inafungua mipaka yake kwa biashara bila Ushuru wa Forodha:-

(a) Je, Tanzania inaathirika vipi na Mkataba huo na ni kiasi gani cha fedha tutapoteza kwa wastani kwa mwaka kutokana na ushuru huo kwa kila nchi yaani kutokana na biashara *(imports)* na jirani zetu Kenya na Uganda?

(b) Kutokana na kupoteza kianzio hicho muhimu, je, Tanzania imeweka mikakati gani ya kiuhakika ya kukabiliana na hali hiyo ili tusiathirike kimapato; na ni vigezo gani vipya vinaweza kuanzishwa kwa lengo hilo?

(c) Je, Serikali inafikiri nini juu ya kushusha *(threshold)* ya milioni 20 kama kigezo cha kuingia kwenye kundi la makampuni ya biashara yanayohusika na *VAT* na ni lini sasa itashusha kiwango cha *VAT* kutoka asilimia 20 cha sasa hadi chini ya 15 kwa lengo la kuvutia biashara na kukuza wigo wa mapato?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha , kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia Mkataba wa *East African Customs Union,* Tanzania itanufaika kwa mambo mengi hususan kushuka kwa bei za bidhaa kwa walaji, pamoja na ushindani wa kibiashara utakaoleta ubora wa bidhaa kwenye jamii yetu ya Afrika Mashariki *(Consumer welfare).* Aidha, kufungua Mipaka yetu kwa biashara bila ushuru wa forodha kutapanua soko la bidhaa zetu zinazouzwa katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa , Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haitapoteza mapato, bali itapata mapato ya ziada ya jumla ya shilingi 5,180,700,000 ziada hii ni tofauti ya hasara ya mapato yatakayotokana na kuondolewa kwa ushuru wa ndani wa jumuiya *(Internal Tariff Elimination)* na ziada itakayopatikana kutokana na uwekaji wa ushuru wa pamoja *(common external tariff).*

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia viwango vya ushuru wa pamoja tulivyo kubaliana baina ya nchi wanachama, Tanzania itapata ongezeko la ushuru wa forodha kwa kiasi cha shilingi 12,864,700,000. Nyongeza hii ya mapato ni kubwa kuliko hasara ya mapato itakayopatikana kwa kuondoa ushuru wa ndani *(Internal Tariff Elimination)* ambao ni shilingi 7,684,000,000 na hivyo kufanya utaratibu mzima wa utumiaji wa ushuru wa pamoja kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na manufaa kwa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Tanzania haiathiriki kimapato kutokana na mkataba huu, Serikali imechukua hatua za makusudi kama ifuatavyo:-

(i) Katika zoezi zima la majadiliano kuhusu kuondoa ushuru wa ndani *(internal tariff elimination),* Serikali imehakikisha kwamba bidhaa zote zenye ushuru mkubwa zinawekwa kwenye daraja (b), *category* ambapo ushuru wake utaondolewa pole pole kwa kipindi cha muda wa miaka mitano ili kutoa fursa kwa Serikali kujipanga upya kuziba pengo kama litatokea.

(ii) Serikali imeunda Tume ya kitalaamu itakayoangalia mapungufu yanayojitokeza na kutoa mapendekezo kuhusu namna bora Tanzania itaendelea kunufaika kwenye mkataba huu, ili hatua za haraka zichukuliwe pale inapobidi.

(iii) Mheshimiwa Spika, Serikali pia imehakikisha kwamba chini ya Mkataba huu bidhaa nyingi zitakazoingia nchini kutoka Kenya zitaendelea kutozwa ushuru wa forodha kwa kiwango cha Kimataifa ambacho kitapunguzwa taratibu kila mwaka mpaka kufikia kiwango cha sifuri kwa muda wa miaka sita ijayo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatafakari uwezekano wa kupandisha kiwango cha chini cha mauzo kwa mwaka kwa ajili ya ya kujiandikisha atika mfumo wa kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kutoka kiwango cha sasa cha shilingi milioni 20 kwenda kiwango cha shilingi milioni 40 na siyo kupunguza *threshold* kama Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, alivyouliza katika swali lake la msingi. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa gharama ya kuwafuatilia walipa kodi wadogo wadogo ambao wanachangia kiasi kidogo cha mapato yatokanayo na *VAT* ambayo ni kama asilimia 5 tu au wakati mwingine huishia kuwa na kodi kubwa ya *VAT* kwenye manunuzi *(input tax)* kuliko kwenye mauzo *(output tax)* na hivyo kudai malipo makubwa ya marejesho *(VAT refund).*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Serikali ni kuboresha mfumo mzima wa usimamizi wa kodi la Ongezeko la Thamani ili kukuza ridhaa ya ulipaji kodi kwa hiari *(voluntary compliance)* ambayo kiwango chake ni kidogo sana kwa saa hapa Tanzania ni asilimia 65 tu ikilinganishwa na viwango vya Kimaitafa. Suala la la kupunguza kiwango cha *VAT* litafikiriwa endapo jamii ya walipa kodi wetu itaanza kulipa kodi ya Ongezeko la Thamani kwa hiari na Serikali kupata mapato yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kodi yanayotokea kutokana na kufutwa kwa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazotoka ndani ya Jumuiya na kuendelea kupunguzwa viwango vya ushuru wa forodha wa kimataifa, kodi zetu za ndani, ikiwemo kodi ya Ongezeko la Thamani, ndizo kodi pekee zitakazotuwezesha kufidia hasara ya mapato yatokanayo na mabadiliko ya mfumo mzima wa ushuru wa forodha. Kwa hiyo, si busara kushusha kiwango hicho kwa wakati huu.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Kwa mujibu wa kanuni za *economics;* na kwa kuwa sisi Kagera ndiyo tunapakana na Uganda; na kwa kuwa wanaweza wakatujazia sementi, bia na kadhalika. Je, Serikali iko tayari kuona kwamba na sisi tunaopakana pale japokuwa hatuna viwanda tunaweza kuuza kahawa zetu, ndizi, maharage na kila kitu kule Uganda?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za *economics* ndiyo maana nimempa takwimu sahihi, kwa sababu tulichokifanya tumekifanya kwa uhakika kuhakikisha ni kiasi gani tunapoteza na kiasi gani nchi inapata kutokana na Mkataba huu.

Kwa hiyo, hakuna tatizo juu ya suala hilo. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi tutakuwa tunaangalia kila tunapoendelea, wapi tunakosa na wapi tunapata. Tulichofanya tumekifanya kwa uhakika. Nimekupeni takwimu sahihi tunapata faida kiasi gani na tunapata hasara kiasi gani lakini yote ni kwamba tunapata faida. Madhumuni yetu katika Jumuiya sote ni kwamba tunanufaika hizo nchi zote tatu. Kuhusu kahawa na nini hilo ni soko huria na hivi sasa linafanyika.

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda naomba nimwite Mheshimiwa anayefuata aulize swali lake, Mheshimiwa Ali Said Salim.

Na. 4

**Malipo ya Pensheni kwa Mkupuo**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa wastaafu wengi walilazimika kuchukua malipo yao ya pensheni kwa mkupuo kwa kuepuka usumbufu:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wale wastaafu waliochukua pensheni zao kwa mkupuo na bado wako hai hadi sasa?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kufikiria muda mpya wa malipo ya pensheni za wastaafu?

(c) Kama Tume ya pamoja ya fedha imeshaanza kazi, je, ni maeneo gani yameshaanza kushughulikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, naomba kwanza nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wastaafu wengi walilazimika kuchukua malipo yao ya pensheni kwa mkupuo kutokana na viwango vidogo vya pensheni ya kila mwezi. Aidha, kwa baadhi walikuwa na malengo ambayo yalihitaji fedha nyingi wakati mmoja hivyo ilikuwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na makali ya maisha kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaanza zoezi la kuwatambua wastaafu waliochukua pensheni zao kwa mkupuo ili waweze kurejeshwa katika daftari la pensheni. Wizara yangu ilitoa tangazo kuwataka wahusika kujiorodhesha katika Ofisi za Hazina Ndogo na Hazina Makao Makuu. Inatarajiwa kwamba wastaafu ambao watakuwa wanastahili kulipwa wataanza kulipwa mwezi Julai, 2004. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa pensheni za wastaafu hulipwa katika mihula miwili ya miezi sita sita kwa mwaka, yaani Julai na Januari. Utaratibu huu unalenga katika kudhibiti wizi wa fedha za pensheni. Wakuu wa vituo vya malipo hutakiwa kuwasilisha Hazina taarifa *(returns)* ya hundi ambazo zinakuwa hazijachukuliwa na wahusika hadi zikachacha. Taarifa hizo huwezesha Hazina kufuta majina ya hundi zilizochacha katika daftari la malipo ya pensheni kabla ya kipindi kingine cha miezi sita.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu hudhibiti malipo ya pensheni yasifanyike kwa wastaafu waliofariki na hivyo kuzuia uwezekano wa hundi hizo kuangukia mikononi mwa watu wasio waaminifu. Utaratibu huu usipofuatwa unaweza kuiletea hasara kubwa Serikali kwa kuwalipa wastaafu hewa.

(c) Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Bunge Na. 14 ya mwaka 1996, iliundwa mwezi Juni, 2003 baada

ya Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Muungano Tanzania kuteua Makamishna wa kuiongoza Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, Tume imejiwekea mpango wa kazi wenye malengo makuu mawili; kujijenga kitaasisi na kuweka misingi imara ya kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tume ipo kwenye hatua ya kutafuta/kuchambua taarifa zinazohusu ushirikiano wa kifedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni maandalizi ya kushughulikia maeneo yenye dosari katika ushirikiano huo.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa inaonekana kuwa hawa wastaafu baada ya kumaliza muda wao hasa waliopitia katika nyanja za siasa wanayumba kimaisha, je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba iko haja ya Serikali kufikiria namna bora ya kuwaenzi watu hawa ili wasiadhirike katika jamii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kila mwaka wakati wa Bajeti huwa tunafikiria namna bora ya kuboresha wafanyakazi wastaafu kwa kuondoa ile fursa ambazo hazikimu maisha yao. Lakini hata hivyo utakuta kwamba inategemea na hali yetu ya kiuchumi vile vile. Utakuta kwamba mwaka jana tumeondoa shilingi 20,000 na tumeondoa mpango wa wastaafu kwa mkupuo kutokana na sheria yenyewe. Kwa hiyo, kila tunapoendelea Serikali itazidi kuangalia namna gani tunaweza kuboresha maisha ya wastaafu.

Na. 5

**Mafunzo ya Usindikaji wa Vyakula na Nembo ya *TBS***

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (k.n.y. MHE. JANET B. KAHAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na ari ya kuviwezesha vikundi vya wanawake na vijana ili waweze kujitegemea kwa kuanzisha biashara ndongondogo, taasisi mbalimbali ikiwemo *SIDO* zimesaidia katika kutoa mafunzo ya usindikaji wa vyakula na kwa kuwa vikundi hivyo vimeshindwa kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi kutokana na bidhaa hizo kukosa nembo ya *TBS:*-

(a) Je, ni viwango gani vinahitajika katika kutimiza masharti ya uthibitishwaji wa kupewa nembo ya *TBS?*

(b) Kama vipo vikundi vya wanawake na vijana, je, vimethibitishwa na *TBS* na ni vikundi vingapi, viko Mikoa ipi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika la Viwango husimamia viwango katika nyanja zote za uchumi wetu vikiwemo viwango vya vyakula vinavyosindikwa na akinamama waliopewa mafunzo ya usindikaji wa vyakula na *SIDO*. Bidhaa za vyakula vinavyosindikwa na vikundi vidogo vya akina mama ni pamoja na mvinyo unatokana na matunda, jamu, sosi ya nyanya na pilipili, chachandu na kadhalika. Viwango vinavyohitajika katika kutimiza masharti ya *TBS* ni pamoja na usafi wa vyumba bidhaa zinapotengenezwa, usafi wa vifaa vinavyotumika pamoja na usafi wa wafanyakazi wenyewe.

Vile vile pamoja na kupima bidhaa husika na kuhakikisha kuwa imekidhi matakwa ya kiwango kilichowekwa kwa bidhaa hiyo. Masharti haya yakitimizwa *TBS* hutoa leseni ya kutumia alama ya ubora ya *TBS*. Nembo ya ubora ya *TBS* hutolewa bure kwa vikundi vya wanawake kama mchango wa Shirika la Viwango Tanzania kwa akina mama wanaotimiza masharti ya ubora.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo vikundi vingi vya akinamama katika sehemu mbalimbali za nchi, ni kikundi kimoja tu kimepata nembo ya *TBS*. Kikundi hicho ni *Ubiri Women Group* cha Lushoto Mkoani Tanga. Kikundi hiki husindika jamu. Pia vipo vikundi viwili ambavyo vimeomba kutumia alama ya ubora ya *TBS*. Vikundi hivi ni Kivumbui cha Arusha ambacho hutengeneza mvinyo wa matunda na Montesori kilichopo Lushoto, Tanga ambacho pia hutengeneza mvinyo wa matunda.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa *TBS* itaendelea kutoa nembo yake ya ubora kwa vikundi vya wanawake wote wanaotimiza masharti ya ubora bila kuwatoza ada kama mchango wa *TBS* katika kuendeleza shughuli za wanawake. Licha ya kusimamia viwango, *TBS* hutoa mafunzo ya ubora kwa vikundi vya wanawake mara tu Shirika linapokaribishwa. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini naomba niulize swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa wanawake na vijana wengi wapo Vijijini na *SIDO* imejitahidi sana katika kuwasaidia mafunzo. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuandaa angalau kitengo maalum ambacho kinaweza kuwasimamia akinamama hawa katika uboreshaji wa bidhaa huko huko Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa mawazo mazuri, lakini ningependa kumhakikishia Mbunge kuwa *SIDO* imekwishaandaa kitengo hicho kwa kusaidiwa na *UNIDO* na sasa hivi tumeweka trainers kila Mkoa. Tumekwishawapatia usafiri baadhi ya Mikoa kufuatana na sera ya *SMMI* na

tutakuwa tayari kusimamia shughuli za akinamama kuwaelewesha na pia kuwaelekeza kwenda *Tanzania Bureau of Standards* ili waweze kupimiwa bidhaa zao kwa ajili ya kupata nembo na hatimaye kuuza katika masoko mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naomba niishukuru Serikali kwa kusaidia wananchi katika masuala mazima ya utengenezaji wa vyakula, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa *TBS* imewekwa pale kuweka ubora wa vyakula na vitu mbalimbali siyo tu kutoka nje na ndani ya nchi kwa afya ya wananchi. Je, hatuoni kwa kutokulazimisha watengenezaji wa vyakula ndani ya nchi wapate nembo ya *TBS* tunaweza kuathiri afya za wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Mbunge kuwa watu wanaotengeneza vyakula wanaweza kuathiri afya za wananchi, *TBS* imejiwekea mikakati maalum ya kufuatilia kila mzalishaji kuhakikisha kwamba anayo nembo ya *TBS.*

Mheshimiwa Spika, zoezi limekuwa gumu kwa mwaka wa kwanza lakini tutahakikisha kwamba tunafuatilia ili kuhakikisha kuwa vyakula vyote vinavyotengenezwa nchini vinapata nembo ya *TBS.* Kwa pale ambapo wananchi wanashindwa, *TBS* hutoa huduma hiyo bure na napenda tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa *TBS* ni mwanachama wa Shirika la Viwango Duniani *(ISO)* na tunafuata kabisa taratibu na masharti ya *ISO* katika kuhakikisha kwamba vyakula vyetu vinafikia ubora unaotakiwa. *(Makofi)*

Na. 6

**Bei Kubwa ya Saruji Nchini**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA (k.n.y. MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB)** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kutokomeza umaskini nchini pamoja na mambo mengine, Serikali imepania kuwasaidia wananchi kupata nyumba bora za kuishi na kwa kuwa saruji ni kitu kimojawapo muhimu katika ujenzi wa nyumba bora na kwa kuwa bidhaa hiyo ni ghali sana hadi sehemu nyingine nchini bei imefikia shilingi 15,000/= kwa mfuko mmoja na kusababisha wananchi walio wengi kushindwa kujenga nyumba za aina hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupunguza bei ya saruji nchini ili wananchi walio wengi waweze kuinunua?

(b) Je, kwa nini Serikali haijengi Viwanda vya Saruji angalau Kikanda kama vile Kanda ya Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa na kadhalika ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo nchi nzima?

(c) Kama Serikali haina uwezo wa kufanya hivyo, je, kwa nini haiwashawishi wawekezaji kufanya hivyo hasa ikizingatiwa kuwa bidhaa hiyo ina uhakika wa kupata soko?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bei ya bidhaa yoyote hutokana na upatikanaji, mahitaji na gharama mbalimbali zinazojumuishwa katika kutengeneza na baadaye kuifikisha bidhaa husika kwa mlaji. Sababu kubwa kuhusu bei ni mjengo wa gharama. Iwapo gharama ni kubwa ni wazi bei ya bidhaa husika itakuwa juu. Katika uzalishaji wa bidhaa kiwandani mjengo wa gharama unatokana pamoja na bei ya malighafi na upatikanaji wake, gharama za umeme na maji na gharama za usafirishaji ili kufikisha bidhaa sehemu inapohitajika.

Baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali inaona umuhimu wa kupunguza bei ya saruji ili wananchi waweze kuitumia, sera zetu ni kwamba Serikali haipangi bei. Bei hufuata mwenendo wa soko. Bei kubwa ya saruji inatokana na gharama zinazohusiana na uzalishaji ikiwa ni pamoja na kupanda kwa gharama ya nishati. Nishati za mafuta na umeme ni karibu asilimia 60 ya gharama za uzalishaji wa saruji. Ili bei ya saruji iteremke Serikali itabidi itoe ruzuku kwa wazalishaji wa saruji jambo ambalo ni gumu kutekeleza kutokana na makubaliano ya Kimataifa na ufinyu wa Bajeti.

(b) Serikali kwa sasa imejitoa kushiriki moja kwa moja katika uzalishaji au biashara. Viwanda vya Saruji hujengwa mahali ambapo pana malighafi nyingi ya *limestone* na pia kuwepo kwa umeme wa uhakika na wa kutosha. Tarifa zilizopo zinaonyesha kuwa ukiachia maeneo ya Tanga, Mbeya na Dar es Salaam ambapo tayari vipo viwanda vya saruji, *Limestone* inayopatikana sehemu nyingine siyo ya ubora unaoridhisha kutengeneza saruji. Vile vile ifahamike kuwa karibu asilimia 92 ya malighafi inayotumika kuzalisha saruji ni *limestone.*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kuboresha mazingira ambayo yatawawezesha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza sio tu katika viwanda vya saruji lakini pia katika viwanda vinginevyo. Hii ni pamoja na kutoa taarifa mbalimbali za kiuchumi zinazowawezesha wawekezaji kufanya maamuzi.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa walaji hawalalamikii zaidi viwanda, wanalalamikia saruji yenyewe na inaonekana hali inakuwa mbaya kwa watumiaji na kwa sasa hali inaonyesha kuwa

wafanyabiashara hawapati fursa ya kuleta saruji kutoka nje na uzoefu unaonyesha kuwa saruji ikitoka nje inakuwa rahisi zaidi kuliko hii yetu hapa ndani. Je, ni lini Serikali italainisha masharti ya uletaji saruji ili watu waweze kuleta saruji kutoka nje na wananchi wafaidike? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, sidhani kama wananchi wanalalamikia ubora wa saruji yetu. Hilo kwanza ni suala ambalo ningependa niliweke sawa. Lakini vile vile sidhani kwamba Serikali imepiga marufuku uagizaji wa saruji kutoka nje. Katika soko huria tunaruhusu lakini pia tunalinda viwanda vyetu, kwa hiyo, kuna masharti ambayo tunaweka, wakiyatimiza wanaweza kuingiza saruji yao. Tumepitisha hapa Sheria ya *Antidumping,* tusingependa ije saruji ambayo haina ubora halafu iharibu soko la ndani na viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na majibu yake aliyoyaeleza bei ya saruji ni nafuu kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mbeya, Mikoa mingine ni gharama mpaka mfuko unafikia shilingi 20,000. Kama Serikali haiwezi kuona hili mwenendo huu utakwenda mpaka lini wakati Serikali ina wajibu wa kulitimiza hilo? Je, hatuwezi kufanya mabadiliko sasa ili Serikali iweke ruzuku katika saruji ili sekondari zijengwe na shule za msingi na mambo mengineyo, je hilo haliwezekani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetazama suala hili kwa ujumla hasa tukizingatia kwamba ujenzi ni muhimu na sera zetu ni kwamba kila mtu apate nyumba.

Mheshimiwa Spika, tumefanya utafiti katika Mikoa mbalimbali ili tuwavute wawekezaji waende katika hiyo Mikoa kuwekeza katika masuala ya viwanda vya saruji. Kigoma tumefika tumekuta *limestone* inayopatikana imechanganyika na *Magnesium Sulphate* ambayo haifai kwani kiwango cha *limestone* ni kidogo sana. Tumekwenda katika Wilaya za Bunda, Shinyanga tumetazama tumekuta pia ipo *limestone* lakini imechanganyika na kitu kinachoitwa *Calcium Sulphate* ambayo ukiichoma na ile *limestone* iliyopo inayeyuka mapema, inaharibu lile tanuru na inaweza kuua watu, iliwahi kutokea Zambia.

Baada ya kuona hayo tukafikiria ruzuku lakini kuna Mikataba ya kidunia *WTO* ambayo tunapigania waondoe ruzuku kabisa, kwa hiyo, tunafuatilia sana na kuweka ruzuku, kwa sasa hivi haitawezekana. Tunachoweza kufanya ni kuhakikisha tumeboresha miundombinu na naomba muwe wavumilivu katika Bajeti ya mwaka huu tutasikia barabara zitakavyotengenezwa. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 7

**Tatizo la Umeme Mkoa wa Lindi**

**MHE. BERNARD K. MEMBE (k.n.y. MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa Mikoa michache isiyopata umeme wa Gridi ya Taifa na kwa kuwa gesi ya Songosongo iliyopo Mkoani hapo husafirishwa Dar es Salaam kwa ajili ya kuzalisha umeme:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kiwango cha umaskini katika Mikoa hiyo kinachangiwa na ukosefu wa umeme wa kuaminika na hivyo kukosa wawekezaji wa kuaminika?

(b) Je, ni sababu gani zinazoifanya Serikali isizalishe umeme kutokana na gesi hiyo kwa ajili ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma badala ya kuendelea kung'ang'ania mradi wa *Mnazi Bay* ambao hadi sasa kiwango cha gesi kilichopo hakijathibitika na wala hauna fedha?

(c) Kwa kuwa Benki ya Dunia ilishatoa fedha kwa ajili ya mradi wa *Mnazi Bay* lakini fedha hizo zikahamishiwa Dar es Salaam kwa ajili ya kununua mashine za *Ubungo Power Station* ili kukabiliana na tatizo la umeme lililotokana na ukame. Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha fedha hizo ili kuendeleza mradi wa *Mnazi Bay?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Lindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumesema mara nyingi hapa Bungeni umeme ni miundombinu muhimu ambayo utakapopatikana kwa uhakika utaleta sura mpya katika mchakato wa maendeleo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mradi wa Songosongo ina mipango madhubuti ya kuipatia umeme Miji Midogo na Vijiji vya Kilwa Masoko, Ikwiriri, Kibiti, Utete, Bunge na Vijiji vingine vilivyopo kando kando ya bomba la gesi ya Songosongo. Umeme kwa ajili ya Miji hiyo utazalishwa na Mitambo ya Megawati 4.5 itakayotumia gesi ya Songosongo. Mitambo hii itajengwa katika maeneo ya Somanga Funga. Laini ya msongo wa 33 itajengwa kutoka Somanga hadi Songino, Kilwa Masoko na laini nyingine pia itajengwa kutoka Somanga hadi Utete, Ikwiriri, Kibiti na Bungu kupitia Nyamwage. Fedha za utekelezaji zitatoka Benki ya Dunia.

Hata hivyo mtambo huu na laini hizi zitakazojengwa ni ndogo na isingeweza kufikisha umeme katika Miji ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Mei, 2004 Serikali ilitiliana saini Mkataba wa uzalishaji umeme kwa kutumia gesi ya *Mnazi Bay* na Kampuni ya Artumas *(Production Sharing Agreement)* kwa ajili ya umeme wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na baadaye Tunduru Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Benki ya dunia iliwahi kutenga fedha kwa ajili ya mradi wa gesi ya Songosongo mwaka 1992, lakini benki hiyo ilitoa masharti kwamba lazima wapatikane wabia wengine na pia lazima Shirika la umeme liwe limefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilishindwa kupata wawekezaji wengine ndiyo maana Serikali imekaribisha uwezekaji wa Kampuni ya Artumas katika mradi wa *Mnazi Bay* ambao utagharimu shilingi bilioni 32.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mradi wa *Mnazi Bay* ni mfumo unaofanana kama na mradi wa Songosongo na pia utatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itachukua miezi sita kuanzia Julai, 2004 na awamu ya pili itajengwa kwa mwaka mmoja utakaoishia Desemba, 2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina matumaini makubwa kwamba mradi huu wa *Mnazi Bay* utafanikiwa. Hata hivyo, endapo majibu ya uhakiki wa gesi iliyopo *Mnazi Bay* hayataridhisha, Serikali inakusudia kutumia utaratibu mwingine wa kuwezesha umeme wa uhakika kupatikana katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa wananchi wa Kilwa swali la msingi linaloulizwa ni lini umeme ule utapatikana, tunajua ahadi za Serikali lakini *specifically* lini umeme huo wa Songosongo utapatikana?

Pili, kwa upande wa umeme wa Miji ya Lindi unaotoka *Mnazi Bay* wananchi wa Lindi nao wangependa kujua kwa sababu mwanzoni ilikuwa inasema itatoka Songosongo, sasa *Mnazi Bay* kwenda Songosongo. Je, Waziri anaweza sasa kujitahidi kuwaambia wananchi wa Lindi lini umeme wa Mkoa ule utapatikana wakati wa kipindi cha Awamu ya Tatu au kipindi cha Awamu ya Nne ya uongozi wa Jamhuri ya Muungano? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nadhani nichukue nafasi hii kama ambavyo nimeeleza katika majibu ya msingi, mradi wa umeme wa Songosongo unatarajiwa kukamilika au kutekelezwa katika kipindi hiki cha miaka miwili na mradi wa umeme wa *Mnazi Bay* kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi pia unatarajiwa kutekelezwa ifikapo mwaka 2005 endapo mambo yote yatakwenda sawasawa kama tulivyosema.

Hatua ya kwanza muhimu ni ya uhakiki wa gesi ya *Mnazi Bay,* tuna matarajio kwamba tutapata majibu mazuri na endapo majibu yatakuwa ya kuridhisha kama nilivyosema katika jibu basi ifikapo Desemba, 2005 tunataraji kwamba mradi huu utakuwa umekamilika. Kwa maana ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mradi huu wa *Mnazi Bay* tunautarajia ukamilike katika kipindi hiki, hadi Desemba, 2005 tunatarajia umeme utakuwa umepatikana.

Na. 8

**Ugonjwa wa Malaria**

**MHE. MARTHA M. WEJJA** aliuliza:-

Kwa kuwa Malaria inaua; na kwa kuwa Serikali inajitahidi kupambana na ugonjwa huo kwa hali na mali:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kuagiza dawa za kunyunyizia kwenye vyoo, madimbwi na kwenye kuta za nyumba ili kuangamiza mazalia ya mbu?

(b) Kwa kuwa kazi ya kunyunyiza dawa kwenye maji yaliyotuama ilifanywa vizuri na Halmashauri zote. Je, Serikali haioni kazi iliyofanywa na Halmashauri hizo nchini ilipunguza gharama ya mara kwa mara?

(c) Je, kuna ukweli gani kwamba dawa inayowekwa kwenye vyandarua haifai kwa afya za wanadamu na kwa nini vyandarua hivyo sio imara na havidumu sana na baada ya miezi nane vinaanza kutoboka?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Michael Wjja, Mbunge wa Viti Maalum, CCM, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwamba njia mojawapo ya kupambana na ugonjwa wa Malaria ni kuangamiza mbu kwa kutumia dawa ya kunyunyiza majumbani *(Indoor Spraying).* Hata hivyo njia hii imethibitika kuwa na gharama kubwa kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu na kwamba kazi hii inatakiwa ifanyike mara kwa mara. Kwa mfano, katika mradi wa majaribio ya kunyunyiza dawa ya kuua mbu uliofanyika katika Manispaa za Tanga na Dar es Salaam kwa miaka mitano (1989-1994) zilitumika kiasi cha shilingi milioni 500. Gharama hizi zilionekana kuwa kubwa mno kuweza kuupeleka mradi huu katika nchi nzima na kwamba usingeweza kuwa endelevu.

Hata hivyo, Wizara yangu inaendelea kutumia njia hii wakati wa milipuko kwa maeneo maalum yenye milipuko ya ugonjwa wa malaria.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Martha Wejja kuwa kazi ya kunyunyiza dawa kuua mbu iliyofanywa na Halmashauri zetu ilikuwa nzuri. Hata hivyo kama nilivyosema awali kazi hii ina gharma kubwa mno.

(c) Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zimefanywa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)* kujua athari za dawa za viuatilifu zinazotumika kwenye vyandarua. Mpaka sasa hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kuwa dawa hizi zina madhara kwa binadamu bali imeonekana kuwa dawa hizi zina uwezo mkubwa wa kumwangamiza mbu.

Mheshimiwa Spika, ubora wa chandarua unategemea sana malighafi iliyotumika kukitengeneza chandarua husika. Kwa mfano, vyandarua vya pamba vimedhihirika kuwa imara zaidi ya vyandarua vya nailoni. Wananchi wanashauriwa kununua vyandarua vilivyo imara zaidi.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili yafuatayo:-

Kama kweli dawa ya kunyunyiza ni ghali, kwa nini Serikali isiagize kisha wananchi watakaokuwa na uwezo wawe wananunua wenyewe ili isaidie kuondoa hatari ya mbu wanaozaliana kwa wingi?

Pili, amesema habari ya dawa kwamba wamefanya tafiti za kutosha kuona kwamba dawa inayowekwa kwenye vyandarua ni nzuri. Mimi sikubaliani naye kwa sababu dawa inapowekwa kwenye vyandarua mbu wanakufa binadamu anayeivuta ndani kwenye mwili huoni kama inaweza kuwa ni hatari, mbu afe binadamu atapona? *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Martha Wejja kwamba Serikali inunue dawa hizi na kisha kuziuza kwa wananchi ni wazo zuri lakini nataka nimwarifu Mheshimiwa Wejja kwamba ili tuweze kununua lazima fedha hizo kwanza ziwepo. Kwa hiyo, hapo ndiyo kwenye mgogoro kwamba bado hatujakuwa na fedha za kutosha kununua dawa hizo. Hilo moja. Lakini la pili, unaponunua kama Serikali halafu ukalazimika kuwauzia wananchi tutakumbana na tatizo lile lile kwamba watakaokuwa na uwezo ndiyo watakaonunua lakini wale maskini bado watashindwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hii dawa inayowekwa kwenye vyandarua kama nilivyosema katika jibu langu la msingi si hatari kwa binadamu na ushahidi huu umethibitishwa kwa tafiti kama nilivyosema. Kwa hiyo, Mheshimiwa Martha Wejja kama anasema yeye anadhani hii ni hatari kwa sababu mbu anakufa, nataka nimhakikishie kwamba uzito wa mbu ni mdogo sana ukilinganisha na wa binadamu. Kwa hiyo, dawa hii haina madhara kwa binadamu kwa sababu kiwango chake hakiwezi kuathiri uzito wa binadamu.

Na. 9

**Watanzania Tisa Waliotekwa**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwanzoni mwa mwaka 2003 katika Wilaya ya Mpanda, Tarafa ya Karema, Kata ya Ikola, Kijiji cha Kasangantongwe wananchi Watanzania tisa walitekwa na watu wa nchi jirani na mpaka sasa hawajapatikana licha ya kuwa wananchi wamekuwa wakiulizia mara kwa mara bila kupewa majibu ya uhakika:-

(a) Je, Serikali inaweza kuwajibu wananchi sasa kupitia Bunge hili mahali walipo wananchi hao?

(b) Kwa kuwa wananchi hao walitekwa na watekaji ni wa nchi gani; je, ni akina nani hasa?

(c) Je, Serikali imelishughulikiaje jambo hilo kiitifaki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli pametokea matukio kadhaa katika Wilaya za Nkasi na Mpanda Mkoani Rukwa na hasa Tarafa ya Kalema, Wilayani Mpanda yaliyohusu raia wetu kutekwa na wageni kutoka nchi jirani ya Kongo *(DRC).* Kila mara tukio kama hili likitokea, Serikali yetu huchukua hatua za kufuatilia na kuwarejesha wananchi wetu.

Kwa mfano tarehe 20 Desemba, 2003, watu sita wa Tarafa ya Kalema, Wilayani Mpanda walitekwa. Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa ilichukua hatua za kidiplomasia za kuwasiliana na uongozi wa *DRC* kwa mujibu wa sheria za Kimataifa kwa lengo la kuwarejesha nchini raia wetu waliotekwa. Hatua hizi za kidiplomasia zimewezesha raia wetu wote sita kurejeshwa wakiwa salama.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wapo Watanzania watano wa Tarafa hiyo hiyo ya Kalema, Kijiji cha Kasangantongwe ambao walitekwanyara mwezi Machi, 2003, hao bado hawajarejeshwa. Uchunguzi unaonyesha walitekwa na majeshi ya Waasi ya *DRC* hivyo njia za mawasiliano na waasi zinakuwa sio rahisi. Juhudi za kidiplomasia bado zinafanywa na Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili kuhakikisha raia wetu wanarejeshwa wakiwa salama.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwahakikishia ndugu wa raia wetu waliotekwa kwamba Serikali inachukua hatua zote za kidiplomasia na pia

tumehusisha Shirika la Polisi wa Kitaifa *(Interpol)* ili kuhakikisha kuwa raia wetu hao wanarejeshwa nchini.

**SPIKA:** Kwa kuwa kulikuwa na shughuli za kumwapisha Mbunge mpya Maswali hayakuanza saa 3.00, kwa hiyo, tunaendelea kidogo mpaka saa moja ikamilike baada ya maswali kuanza.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa moja ya mambo ambayo yanachangia na kutokea matatizo haya katika maeneo hayo ni kutokuwepo na mawasiliano ya haraka kutoka maeneo hayo yenye matatizo na kufika kwenye vyombo vyetu ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.

Je, Serikali inafanya nini na inachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba inaimarisha vyombo vya mawasiliano katika maeneo hayo ya Karema, Ikola, Kasanga, Kabwe, Kirando na Mto Wisa ili pindi panapotokea matatizo hayo basi hatua za haraka ziweze kuchukuliwa katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na kuimarisha suala la usafiri pamoja na kuweka boti za doria zitakazofanya doria katika ukanda huo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, eneo hili linalozungumziwa ni eneo la Mpakani, Mpaka wetu na nchi jirani ya *DRC* ambao ni Ziwa na sasa hivi baada ya matokeo haya kutokea Serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti kuimarisha mawasiliano.

Sasa hivi tuna kituo cha Polisi pale Karema tutakipatia *radio call* na vile vile wananchi kwa nguvu zao wenyewe wanajenga kituo kingine cha Polisi eneo la Ikolo na chenyewe tumeshaomba watuletee mahitaji yao ili tushirikiane tukamilishe ili pale napo tuweke kituo cha Polisi na kuweka *radio call.* Juhudi zote hizi ni katika kuimarisha mawasiliano.

Kuhusu boti kwa sababu ule Mpaka ni wa maji tayari Wizara yetu ya Mambo ya Ndani tunakarabati boti ambayo ilikuwa pale Kipili, Namanyere ilikuwa mbovu kwa muda fulani sasa hivi tunaikarabati baada ya muda mfupi itakuwa tayari kusaidia shughuli katika ziwa hilo.

Wizara wenzetu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wameweka pale kiteule *(detachment)* pale Karema na wameshapatiwa boti kubwa yenye *speed* kubwa. Kwa hiyo, kwa juhudi zote hizi za Polisi na Jeshi la Wananchi kupatiwa hizi boti na kuimarisha ulinzi tunataka tuwahakikishie wananchi wa eneo lile kwamba Serikali inachukua kila juhudi kuhakikisha usalama wao. *(Makofi)*

Na. 10

**Tume ya Haki za Binadamu**

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba chini ya Ibara ya 130(1)(a) - (h) hadi 130(6); na kwa kuwa Ibara 130(2) imeeleza wazi kuwa Tume itakuwa ni Idara inayojitegemea na haitalazimika kufuata maagizo au amri ya mtu yeyote na Idara yoyote ya Serikali au maoni ya Chama chochote cha Siasa, Taasisi nyingine yoyote ya umma au sekta binafsi:-

Je, Tume hiyo imeshapokea malalamiko mangapi ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora kwa mwaka 2003/2004; na ni mangapi kati ya hayo yameshapatiwa ufumbuzi na ni mangapi hayajapatiwa ufumbuzi na ni kwa nini?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Katika mwaka 2003/2004 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hadi kufikia tarehe 20 Mei, 2004 ilipokea malalamiko 2,316. Kati ya hayo malalamiko 265 yalikamilika uchunguzi wake na kupatiwa ufumbuzi kama ifuatavyo:-

Malalamiko 23 yalifaulu, malalamiko 16 hayakufaulu, malalamiko 149 yalielekezwa kwa vyombo mbalimbali vyenye mamlaka ya kisheria kuyashughulikia na malalamiko 77 yaliachwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo kukosa ushahidi, swali kutoeleweka na kadhalika. Malalamiko 2,051 yanaendelea kuchunguzwa. Malalamiko haya yanayoendelea kuchunguzwa yamechelewa kukamilika kwa kupatiwa ufumbuzi kwa kuwa walalamikiwa walio wengi *(Respondents)* wanahitaji kufuata taratibu za kisheria ili kupata majibu kutoka mamlaka ili waweze kuijibu Tume. Mfano wa malalamiko hayo ni yale yanayohusu kutopandishwa vyeo, madai ya mirathi na kiinua mgongo au masuala yanayohusu malipo ya pensheni. Sababu nyingine iliyochangia kuchelewa kupatikana ufumbuzi wa malalamiko hayo ni uhaba wa watumishi katika Tume. Tatizo hili linategemewa kumalizika karibuni kwani ndipo sasa Tume imepewa kibali cha kuajiri watumishi kulingana na muundo wake mpya.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Je, Tume imeshawashughulikia vigogo wangapi ambao wametuhumiwa kuvunja Haki za Binadamu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, jumla ya malalamiko ambayo Tume imepokea mpaka sasa hivi kwa Tanzania Bara ni 7,951 na

kwa upande wa Zanzibar ni 133. Yaliyopatiwa ufumbuzi kwa upande wa Tanzania Bara ni 2,886 lakini kwa upande wa Zanzibar bado hayajapatiwa ufumbuzi na hii inatokana na matatizo ya Tume kwa kweli kutokuanza kufanya kazi kwa sababu za kisheria na sasa hivi tunawasiliana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba sheria hiyo inaanza kufanya kazi na hivyo Tume kuweza kufanya kazi Zanzibar.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha kabla hatujaendelea na mambo mengine kuna tangazo moja linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje anawaomba wajumbe wake wafanye kikao saa 4.30 asubuhi hii kwa madhumuni ya kuzungumza na ujumbe wa Wabunge wa Kenya katika Ukumbi wa Na. 231 ghorofa ya pili. Mwisho wa matangazo tunaendelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004
### *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria uitwao *The Written Laws Miscellaneous Amendments Act,* 2004 sasa usomwe Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya mabadiliko katika sheria nane mbalimbali zifuatazo:-

Sheria ya kwanza ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini ya Mwaka 2001 *(The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, 2001),* sheria ya pili ni Sheria ya Mkonge ya Mwaka 1997 *(The Sisal Act of 1997),* sheria ya tatu ni Sheria ya Chai ya Mwaka 1997 *(The Tea Act of 1997),* sheria ya nne ni Sheria ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ardhi ya mwaka 2002 *(The Courts Land Disettlements Act, 2002)* na sheria ya tano ni Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai ya Mwaka 1966 *(The Civil Procedure Code No. 49 of 1966).*

Sheria ya sita ni Sheria ya Udhibiti wa Vyakula, Dawa na Vipodozi ya Mwaka 2003 *(Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act,2003),* sheria ya saba ni Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 *(The Land Act 1999)* na sheria ya mwisho ni *The Audio Visual Institute of Dar es Salaam Act, 1994.*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Kamati yake ya kuchambua Muswada huu na hivyo kuwezesha Muswada huu uwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

Mheshimiwa Spika, sheria ya kwanza inayopendekezwa kufanyiwa mabadiliko ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na wa Majini ya Mwaka 2001. Itakumbukwa kwamba wakati sheria hii ilipotungwa chombo cha *SUMATRA* kilipewa jukumu la kusimamia masuala mbalimbali yaliyoainishwa katika sheria hiyo.

Hata hivyo majukumu hayo hayakujumuishwa udhibiti wa shughuli za uokoaji yaani *(Search and Risk operation).* Usimamizi na ukaguzi wa meli za kigeni zinazoingia katika Bandari zetu yaani *(Port control)* pamoja na uratibu, ukaguzi na usimamizi wa utoaji huduma katika vyombo vya usafiri wa majini pamoja na ubora wa vifaa vya usalama katika vyombo hivyo. Ukosefu wa udhibiti wa shughuli hizi umesababisha kuwepo na udhaifu katika utendaji na utoaji huduma katika vyombo vya usafiri wa majini na udhibiti wa mali zinazoingia katika Bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa vile vile kwamba *SUMATRA* ilipewa majukumu yaliyokuwa yanafanywa na Shirika la *Tanzania Central Freight Bureau (TCFB).* Baada ya shughuli za *TCFB* kuhamishiwa *SUMATRA* kwanza wapo wafanyakazi watakaohamishiwa *SUMATRA* na wengine watakaopelekwa katika Idara nyingine za Serikali na kwingineko.

Pili, yapo majukumu mengine yatakayohamishiwa *SUMATRA.* Vile vile imeonekana ipo haja ya kuweka kinga kwa mali za *SUMATRA* kama ilivyo kwa mali nyingine za Serikali ili mali hizo zisiweze kukamatwa kwa *tanch* za hukumu za Mahakama na badala yake kuwepo utaratibu mbadala wa kulipa madeni yatakayotokana na hukumu halali za Mahakama. Kutokana na mapungufu hayo yaliyojitokeza kati ya utekelezaji napendekeza sheria ya *SUMATRA* ifanyiwe marekebisho katika sheria hiyo kama ifuatavyo:-

Kwanza, inapendekezwa kwamba fungu la sita la sheria hiyo lifanyiwe marekebisho ili kuiongezea *SUMATRA* majukumu ya uratibu wa operesheni za uokoaji yaani *(search and risk of operation),* usimamizi wa ukaguzi wa meli za kigeni zinazoingia katika Bandari zetu *(Port control)* na uratibu na ukaguzi wa utoaji huduma katika vyombo vya usafiri wa majini *(Maritime Security).*

Aidha, inapendekezwa fungu la 14 lirekebishwe ili kumtambua Msajili wa Meli aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usajili wa Meli *(The Maritime Shipping Act)* kuwa mmoja wa Wakurugenzi wanaoshughulikia udhibiti wa shughuli za meli bandarini zilizoainishwa. Marekebisho haya yatawianisha Mamlaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Usajili wa Meli na Udhibiti wa Usafiri Majini. Aidha, kwa kuzingatia uharaka na utaalamu unaohitajika katika utekelezaji wa majukumu hayo inapendekezwa kuongeza fungu jipya la 6(a) ili kumwajibisha Msajili huyo moja kwa moja kwa Waziri mwenye dhamana ya mambo ya Uchukuzi ili maamuzi yake yaweze kutolewa kwa haraka na kwa utaalamu.

Fungu jipya la 48(a) limeongezwa kwa ajili ya kuanisha kwa makini maslahi ya wafanyakazi wa *Tanzania Central Freight Bureau* watakaohamishiwa katika utumishi wa *SUMATRA* na wale ambao utumishi wao utahamishiwa katika Idara na Taasisi nyingine

za Serikali. Kwa wale watumishi wa *Tanzania Central Freight Bureau* watakaohamishiwa *SUMATRA* mahitaji halisi ya *SUMATRA* pamoja na vigezo vyote vya ajira vitafuatwa. Watumishi wengine watakaoajiriwa katika Idara za Serikali na Taasisi zake kama itakavyoonekana inafaa maslahi yao pia yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni mapendekezo ya kufanyiwa marekebisho linahusu upanuzi wa vyanzo vya mapato vya *SUMATRA.* Inapendekezwa kulifanyia mabadiliko fungu 41 la sheria hiyo ili kuiruhusu *SUMATRA* kutoza ada ya huduma ya ukaguzi wa meli.

Sheria ya pili inapendekezwa kufanyiwa marekebisho sheria zinazofuata na zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho yanayofanana ni Sheria ya Mkonge Na. 2 ya Mwaka 1997 na Sheria ya Chai Na. 3 ya Mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuainisha kwa uwazi zaidi uteuzi wa wajumbe wa Bodi hizo. Mabadiliko katika Sheria ya Katani yanapendekezwa kufanyika katika ibara ya 1 jedwali la Sheria ya Mkonge inayoelekeza uteuzi wa wajumbe wa Bodi ambapo kuna aina tatu za wajumbe.

Kundi la kwanza Mwenyekiti na wajumbe wa kati ya wawili na wanne wanaoteuliwa kutokana na mapendekezo ya Waziri miongoni mwa watu wenye uzoefu na waliobobea katika taaluma zao. Kundi lingine ni wajumbe wengine wawili wanaoteuliwa na vyama vya wakulima wa Mkonge na kwa upande wa zao la chai vyama vya wakulima wa chai. Aina hii ya tatu ya wajumbe haielezwi inateuliwa kwa utaratibu upi. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika ibara ya 1(c) ya jedwali ya Sheria ya Mkonge ili kuelekeza bayana kwamba wajumbe hao watateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa majina yasiyopungua mawili au kuzidi matano yatakayopendekezwa na chama cha wakulima wa Mkonge.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Chai pia inarekebishwa ili kuanisha upya wajumbe wa Bodi. Muundo mpya wa Bodi umezingatia uwakilishi wa wadau wote yaani wakulima wadogo, Chama cha Wakulima wa Chai wenye viwanda vya chai na Serikali. Aidha, Afisa Mtendaji wa Bodi ndiye atakuwa Katibu wa Bodi. Waheshimiwa Wabunge, naamini mtakubaliana nami kwamba kwa mabadiliko haya sasa Bodi hizi zimewekwa mikononi mwa wenyewe kwa uwazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya nne inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni ya usuluhishi wa migogoro ya ardhi *(The Courts Land Disettllement Act).* Inapendekezwa kwamba Wenyeviti wa Mahakama za Ardhi za Wilaya waapishwe na Jaji wa Mahakama Kuu kabla ya kushika madaraka yao badala ya utaratibu uliotajwa katika sheria hiyo ya kuapa mbele ya Wakuu wa Mikoa. Utaratibu huu wa Wenyeviti wa Mabaraza haya ya kuapa mbele ya Mkuu wa Mkoa unakiuka dhana ya mgawanyo wa Madaraka pamoja na uhuru wa Mahakama. Mahakimu Wakazi watakaoteuliwa kuwa Wenyeviti wa Mahakama za Ardhi za Wilaya watabaki katika viapo vyao walivyoapishwa na Jaji Mkuu. Kwa maneno mengine hawatatakiwa kuchukua kiapo kingine.

Mheshimiwa Spika, sheria ya tano inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni ya udhibiti wa vyakula, dawa na vipodozi ya mwaka 2003 *(The Tanzania Food, Drugs*

*and Cosmetics Act of 2003).* Mabadiliko yanayopendekezwa ni kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya Sheria ya Wakala wa Serikali inayokataza Watendaji Wakuu Wakala wa Serikali kuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi husika. Sasa hivi kwa mujibu wa sheria hiyo Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Udhibiti wa Vyakula, Dawa na Vipodozi pia ni Mjumbe wa Bodi. Inapendekezwa kukifuta kifungu cha 1(c) ili kumwondoa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi kuwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya sita inapendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Uendeshaji wa Mashauri ya Madai Na. 49 ya mwaka 1966. Madhumuni ya marekebisho haya ni kusisitiza zaidi kwamba amri za muda za Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Wakazi na Mabaraza mengine ambayo rufaa zake zinasikilizwa na Mahakama Kuu zisikatiwe rufaa mpaka kesi ya msingi itakapoamuliwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba mwaka 2002 Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria namba 25 ya mwaka 2002 iliyokataza amri za muda zinazotolewa na Mahakama za Mahakimu kukatiwa rufaa. Katika sheria hiyo hazikutajwa amri za namna hii zinazotolewa na mabaraza mbalimbali yaani *Tribunals.*

Mabadiliko yanayopendekezwa kufanywa katika fungu la 74 (1) yana lengo la kupanua wigo ili kuzuia rufaa za amri za muda zinazotolewa na Mabaraza yaani *Tribunal* ambayo maamuzi yake yanakatiwa rufaa Mahakama Kuu. Madhumuni ya marekebisho haya ni kuhakikisha kwamba kesi zinazofikishwa Mahakamani ziamuliwe haraka kwa misingi ambayo waliofika Mahakamani kuomba haki ndicho wanachokitafuta.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya saba inayopendekezwa kufanyiwa mabadiliko ni Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999. Inapendekezwa marekebisho katika fungu la 19 ili kuwaruhusu kumiliki ardhi wageni wanaokuja kuwekeza nchini katika huduma za jamii, elimu au afya, masuala ya kupambana na umaskini na ya maendeleo ya jamii. Vile vile marekebisho haya yana shabaha ya kuruhusu Balozi za nchi za nje, Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama kuweza kumilikishwa ardhi. Itakumbukwa kwamba sheria ya ardhi ilipopitishwa ilifanyika jitihada kubwa kulinda maslahi ya wananchi kwa kuweka masharti magumu kwa wageni kumiliki ardhi nchini. Masharti hayo yalikuwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wageni wanatimiza masharti ya uwekezaji kupitia *Tanzania Investments Centre (TIC).*

Katika utekelezaji wa sheria hii imedhihirika kwamba masharti yaliyowekwa ya kulinda ardhi kwa manufaa ya wananchi wakati mwingine yanawanyima wananchi faida na fursa ya maendeleo na huduma. Kwa mfano, masharti hayo yameziba kabisa milango kwa Taasisi na Mashirika ya kutoka nje ya nchi ambayo yanachangia katika kutoa huduma kwa umma za kupambana na ujinga, maradhi na umaskini kwa kutoa elimu, huduma za afya, maji na kadhalika.

Aidha, imekuwa vigumu kwa Serikali kutimiza majukumu yake ya kutoa ardhi kwa Balozi za nchi za nje na Mashirika ya Kimataifa ambayo nchi yetu ni wanachama. Jambo ambalo ni muhimu katika kudumisha ushirikiano wa nchi yetu na Mataifa mengine. Hivyo ili kuondoa kikwazo hicho inapendekezwa kukifanyia marekebisho

kifungu cha 19 cha sheria ya ardhi ya mwaka 1999 ili kutoa fursa ya kumilikisha ardhi kwa taasisi zinazoshirikiana na Serikali katika kupambana na umaskini, ujinga na maradhi au kueneza dini kwa maslahi ya wananchi wetu.

Aidha, Serikali za nje zenye Balozi hapa nchini na Mashirika ya Kimataifa ambayo Tanzania ni mwanachama pia zipewe fursa hiyo ya kumiliki ardhi.

Mwisho inapendekezwa kwamba Bunge lako Tukufu liridhie kufutwa Sheria ya Vielelezo ya mwaka 1974. Taasisi ya Vielelezo hivi sasa haipo tena, majukumu yake tayari yanatekelezwa na Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa mwaka 1997. Kwa maneno mengine Sheria ya Taasisi ya Vielelezo ya mwaka 1974 sasa haihitajiki tena.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kukushukuru tena wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Muswada huu na kupitia kwako nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nina wasemaji wawili tu Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa William Shellukindo. Lakini orodha bado iko wazi. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Muswada huu au mwakilishi wa Kamati, Makamu Mwenyekiti atoe maoni ya Kamati hiyo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 70(2), Toleo la Mwaka 2004 naomba kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala nitoe maoni kuhusu Muswada wa Sheria uitwao *The Written Laws Miscellanuous Amendments Act, 2004.*

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo naomba kwanza uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge kwa kurudishwa tena Bungeni kwa mara ya pili. Ushindi wake umeonyesha ni kwa kiasi gani wananchi wa Jimbo la Bariadi Mashariki walivyo na imani naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambao walichambua hadi kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru,

Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni namba 93 kifungu kidogo cha kwanza, Kamati yangu inasimamia Wizara zifuatazo: Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Katika kusimamia Wizara hizo, Kamati yangu imepewa majukumu yafuatayo kwa mujibu wa kanuni namba 93 (2) 2004: Kwanza ni kushughulikia Bajeti ya Wizara hizo. Pili, kushughulikia Muswada wa Sheria na mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo. Tatu, kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo na nne, kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni namba 69 (1) Toleo la 2004, Kamati yangu ililetewa Miswada ya kurekebishwa sheria nane kama ifuatavyo: Sheria ya kwanza ni *Surface and Marine Transport Regulatory Authority, 2001.* Sheria ya pili ni *Sisal Industry, 1997.* Sheria ya tatu ni *Tea Industry, 1997.* Sheria ya nne ni *Courts, Land Disputes Settlements, 2002.* Sheria ya tano ni *Tanzania Food, Drugs and Cosmetics, 2003.* Sheria ya sita ni *Civil Procedure Code, 1996.* Sheria ya saba ni Sheria ya Ardhi, 1999 na sheria ya nane ni *Audio Visual Institute of Dar es Salaam, 1974.*

Kamati yangu ilikuwa na maoni yafuatayo: Kwenye Muswada wa kwanza, *Surface and Marine Transport Regulatory Authority,* katika sheria hii marekebisho yalihusisha kuongezwa majukumu mapya kwa Mamlaka ya *SUMATRA,* namna ya ajira kwa ngazi mbalimbali za utendaji katika *SUMATRA*, vyanzo vya mapato na kadhalika. Wajumbe walikubaliana na mapendekezo hayo ingawa walitaka kujua iwapo katika shughuli za uokoaji *SUMATRA* yenyewe itakuwa na vifaa vya uokoaji. Tunashukuru Serikali kuliona hilo kuwa itabidi *SUMATRA* iwe na vifaa hivyo la sivyo italazimika kukodisha kutoka kwa walio navyo. Pia, Wajumbe walitaka sheria itamke wazi kuhusu hali iwapo kunatokea janga lolote, Mashirika ya Uokoaji yanataka yalipwe fedha kwanza ndipo yashughulikie janga hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria namba mbili ya *Sisal Industry,* Kamati yangu ilikubaliana na marekebisho yote yaliyopendekezwa na Serikali. Pia, kuhusu sheria ya tatu ya *Tea Industry,* Kamati yangu ilikubaliana na marekebisho yote yaliyopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya nne ambayo ni *Courts, Land Disputes Settlements, 2002,* marekebisho yalihusu ni kwa mamlaka ipi Mwenyekiti wa Baraza la

Ardhi la Wilaya aape. Katika sheria ya awali ilitakiwa Mwenyekiti huyo aape kwa Mkuu wa Mkoa. Hali hii ilileta ugumu hasa kwa Wenyeviti ambao watakuwa Mahakimu. Hivyo, katika marekebisho haya, Wenyeviti siyo lazima wawe wataalam wa sheria, lakini watakula viapo vyao kwa Jaji Mkuu wa Mahakama na kwa Mahakimu hawatalazimika kula kiapo upya. Kamati yangu imefurahishwa na tarifa kuwa Jaji Mkuu tayari ameteua Mahakimu 20 na kuwapeleka Wizara ya Ardhi, ambapo watakuwa Wenyeviti wa Mabaraza hayo na hivyo kumaliza tatizo hilo la Wenyeviti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya tano, *Tanzania Food, Drugs and Cosmetics,* Wajumbe walikubaliana na mapendekezo na marekebisho hayo ya Serikali. Sheria ya sita ni *Civil Procedure Code, 1996,* katika sheria hii ilikuwa ni kufanya marekebisho ili kusiwepo mianya ya kucheleweshа kesi kiujanja ujanja. Kamati yangu ilikubaliana na marekebisho hayo na hivyo marekebisho hayo yatamaliza au yatapunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa kesi.

Mheshimiwa Spika, sheria namba saba ni Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Katika marekebisho haya ilikuwa ni kuongeza aina ya watu au Taasisi zinazoruhusiwa kumiliki ardhi Tanzania. Katika sheria ya mwanzo, mtu yeyote asiye raia hakuruhusiwa kumiliki ardhi, lakini sheria haikutamka kuhusu Mashirika na Taasisi za nje au ndani zisizo za kibiashara ambazo zina lengo la kutumia ardhi hiyo kwa lengo la kutoa huduma za elimu, afya na kidini, zenye lengo la kuondoa umaskini kwa wananchi, wapewe ardhi hiyo bila kupitia kwanza *Tanzania Investment Centre.* Kamati yangu ilikubaliana na marekebisho hayo lakini kwa tahadhari kuwa baadhi ya Taasisi zinaweza kutumia mianya hiyo kujipatia ardhi na hatimaye ardhi hiyo kutumika kwa malengo tofauti. Pia, Kamati yangu ilitahadharisha kuwa kuna uwezekano wa kutaka kupata ardhi kubwa kuliko mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya nane ni *Audio Visual Institute of Dar es Salaam, 1974.* Katika marekebisho haya lengo ni kuifuta Taasisi hii kwa vile shughuli zake sasa zinasimamiwa na kuendeshwa na Wakala wa Serikali wa Tume ya Utangazaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hayo, naomba sasa nitoe mapendekezo yafuatayo kuhusiana na marekebisho hayo: Serikali iwe makini wakati wa kutoa ardhi kwa Taasisi zilizoongezwa ili kuepusha matumizi mabaya ya nafasi hiyo. Pia, kwenye sheria hiyo kuwepo na kipengele ambacho kitampa madaraka Waziri wa Ardhi kufuta umiliki wa ardhi kwa ardhi hiyo pindi itakapogundulika kuwa ardhi hiyo haitumiki kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi ya kutoa maoni ya Kamati. Napenda pia nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa umakini wake katika sheria hata kuleta marekebisho ambayo tunayaona yataleta mafanikio makubwa katika Sekta husika. Napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu na Katibu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, waliozipitia kwa umakini mkubwa sheria hizi na hivyo kutoa mchango mkubwa wa kuziboresha. Pia, napenda niwashukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Musa na Makatibu wa Kamati, Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Aggrey Nzowa, kwa huduma mbalimbali walizotoa kwa

Kamati hii hata ikafanya kazi nzuri.  Mwisho, nawashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu marekebisho ya sheria ndogo ndogo *(Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2004).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 43(b)(c) Toleo la 2003, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Kamati zilizomaliza ziara na vikao mbalimbali wiki iliyopita.  Vile vile,  kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kudondoa mapungufu yafuatayo Kamati iliyoyabaini katika Sheria zifuatazo ambazo zinafanyiwa marekebisho: Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini, 2001 *(The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act, 2001)* katika kifungu cha sita kinachoongeza kazi za Mamlaka kwa pamoja na kudhibiti meli za kigeni, sheria hii haijaainisha meli za hapa nchini zitadhibitiwa na nani.  Kifungu kipya cha 48(b)cha Muswada huu kinapendekeza kuweka kinga ya mali za Mamlaka kuwa zisihusishwe katika utekelezaji wa hukumu za Mahakama na badala yake Mkurugenzi alipe kiasi cha fedha kutoka kwenye Mamlaka kwa ajili ya madai ya Mahakama au hukumu.

Mheshimiwa Spika, hii inaashiria kwamba, Mamlaka hii itakuwa juu ya sheria na inapingana na Katiba.  Kuna hatari ya watendaji wa Mamlaka hiyo kutumia mwanya wa sheria hii kuwanyima watu haki zao.  Hii haijapendekeza njia mbadala ya kuwalipa watu watakaopewa hukumu halali za Mahakama iwapo itakosa pesa taslimu za kuwalipa.  Jinsi ilivyo inatoa mwanya kwa Mamlaka kutowalipa wadai wake kwa kisingizio cha kutokuwa na fedha taslimu za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulikusudia kupendekeza mabadiliko fulani baada ya kifungu cha 48(b) lakini hakikuorodheshwa.  Hapa inasomeka: *“By adding immediately after section 48(b) as added the following...”* Hakuna chochote kilichoongezwa, hivyo ni mwanya pia wa kuongeza chochote baada ya sheria kupita. Tunataka vitu hivyo viwe wazi kwa kila mtu kuelewa.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ubadilishaji wa *Sisal Act, 1997,* awali kabla ya mabadiliko hayo *Sisal Industry Act* inasema: "Kati ya Wajumbe wa Bodi kutakuwa na Wajumbe wawili walioteuliwa na *Sisal Association of Tanzania.*"  Marekebisho yametaja

kuwa Waziri anaweza kuteua wawakilishi wawili kutoka kwenye orodha atakayopewa ambayo ni kati ya watatu na siyo zaidi ya watano. Hii inakanganya, uhuru wa kujichagulia au kuteua wawakilishi wake kama kifungu kipya (c) kinavyoeleza, nanukuu: *"Two representatives of a Sisal Association of Tanzania appointed by Minister from amongst not less than three and not more than five nominated persons."*

Mheshimiwa Spika, sheria hii bado haifafanui ni chombo au mtu gani anapendekeza majina ya watu ambao Waziri atateua wawili kati yao kuwa Wajumbe wa Bodi. Tunaomba ufafanuzi ili na wale wahusika wawe wazi na kazi hii. Vile vile, kwa ajili ya uwajibikaji zaidi kwa Wajumbe wa Bodi, tunapendekeza Wizara husika itangaze kwenye Vyombo vya Habari na iweke vigezo vinavyotakiwa ili Wajumbe wote waombe nafasi ya kuwa Wajumbe wa Bodi na wafanyiwe usaili. Kumbukumbu zao za utendaji kwa miaka ya nyuma kiwe ni kigezo ili kuondoa tabia ya ubadhirifu na kutoheshimu watu waliowaweka kwenye madaraka hayo na wale wanaowatumikia. Baada ya kupatikana washindi kwa njia ya usaili *(interview),* basi watangazwe kuwa wao ndiyo Wajumbe wa Bodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Tea Act Number 3 of 1997*, Muswada huu unapendekeza kufuta jedwali la kwanza la Sheria ya Chai Na. 3 ya 1997, linalotoa muundo wa Bodi ya Wakurugenzi wa Chai. Hata hivyo, kifungu cha 2(1)(b) cha Muswada huu, hakielezi nani anapendekeza Wajumbe watatu mpaka watano wa Bodi hiyo watakaotoka kati ya wakulima wadogo wadogo ambao wawili miongoni mwao watateuliwa na Waziri kuwa Wajumbe wa Bodi hiyo ya Chai.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi hiyo wapatikane kwa njia ya usaili kwa vigezo ambavyo vitawekwa na Wizara na nafasi hizo zitangazwe kwenye Vyombo vya Habari na Waziri mhusika. Kabla ya usaili, kumbukumbu za utendaji wao wa nyuma uhakikiwe kabla ya kupewa nafasi hizo ili kupunguza ubadhirifu wa utendaji wao mbovu utakaohatarisha Mamlaka hii.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na uwiano wa wawakilishi kati ya wadau wa chai na Wajumbe wengine ili kuwe na uwiano kwenye maamuzi yanayohitaji kupigiwa kura. Hata hivyo, idadi ya wawakilishi wa wadau wa chai waongezwe hadi wanne kuepusha maamuzi kutegemea upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kudondoa hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza mjadala wa jumla, lakini niwataarifu kwamba, kuna karatasi ya marekebisho ambayo tumeigawa wakati wa maswali. Kwa hiyo, mjadala uzingatie vile vile marekebisho hayo.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya awali ili nami niweze kujadili Muswada huu wa kurekebisha sheria mbalimbali. Kabla ya hapo naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wananchi wa Mbulu,

kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bariadi Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama ili kuchangia maeneo mawili tu katika Muswada huu na maeneo yenyewe yanahusu masuala ya ardhi na ninapata faraja kubwa sana kwa sababu ninamwona Waziri wa Ardhi naye yupo hapa na haya nitakayosema nina hakika atayazingatia katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, suala la kuapa mbele ya Jaji, halinipi matatizo yoyote, isipokuwa tu kama ndiyo mgao wa majukumu ya Serikali ifahamike pia kwamba mashauri haya yanaanzia kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji na lile Baraza la Kata limeundwa chini ya Sheria ya Mabaraza ya Kata ya Mwaka 1984 na Baraza la Ardhi la Kijiji, nafikiri uhai wake unatokana na Sheria Namba Nane ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982. Nafikiri hili pia Mwanasheria Mkuu anapaswa kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo madogo sana, lakini jambo la msingi ambalo nadhani ni lazima tulijadili tupende au tusipende, hivi kweli kuna maana yoyote juu ya kuwepo kwa Baraza la Ardhi la Kijiji, Baraza la Ardhi la Wilaya , Baraza la Ardhi na Nyumba la Mkoa? Kuna mashauri mamia na mamia yamekwama katika maeneo hayo yote, hakuna jambo lolote linalotendeka sasa hivi katika maeneo hayo yote na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, mashauri haya sasa hayapelekwi tena kwenye Mahakama ya kawaida. Kati ya mwaka 1992 hadi leo katika Wilaya ya Mbulu, Wilaya ambayo mimi natoka, kuna mashauri yasiyopungua 100 ambayo yamekwama Wilayani, yemekwama kwenye Kijiji na kwenye Kata, kwa sababu hakuna Baraza la Kata linalofanya kazi. Sasa hii ni vurugu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, mabaraza haya hayafanyi kazi kwa sababu moja, pesa. Mabaraza ya Kata hayafanyi kazi kwa sababu hakuna pesa. Katika kikao fulani cha Mkoa, Wilaya fulani ilitaka kuanzisha Mabaraza yao upya ili pesa ya kuziendesha zipatikane kutokana na faini. Haya ni mambo ya zamani, eti uendeshe mabaraza haya kutokana na faini zitakazopatikana kutokana na uendeshaji wa mashauri haya! Sasa hii ni nini, tunaenda wapi katika karne ya 21?

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu pengine utatuwezesha kupata muundo muafaka, kwa sababu sheria hii inataja wanawake wanne na wanaume wanne kuwa katika Baraza lile na Mwenyekiti. Katika Serikali za Vijiji sasa hata uwiano huo haupatikani. Kwa hiyo, bila shaka katika uchaguzi wa baadaye mwaka 2005 hali hii itarekebishika, lakini sasa fedha za Katibu wa Baraza zitapatikana wapi? Pengine Katibu wa Baraza sasa atakuwa Katibu wa Kijiji au Mtendaji wa Kijiji. Tumeambiwa atalipwa na Serikali, kama ndiyo hivyo angalau sasa tutakuwa na ahueni.

Sasa wale Wazee wa Baraza watalipwa na nani? Tunataka kukaribisha rushwa tena katika eneo nyeti kama la ardhi. Nimesema katika Kata hamna kitu kwa sababu hakuna fedha, Mabaraza yale hayafanyi kazi, hayapo. Kwa vyovyote vile itakuwa hamna mantiki, hamna *logic* ya rufaa kutoka kwenye ngazi ya chini mpaka Wilayani, mpaka kwenye Mkoa na mpaka mwenye Mahakama ya Ardhi. Waziri na Mwanasheria Mkuu

wa Serikali walielewe kabisa suala hili, tunafanya nini kama shauri linaanza kwenye Baraza la Kijiji na hapa katikati hakuna mahali pa kukata rufaa? Baraza la Wilaya halipokei rufaa kutoka Kijijini, linapasa kupokea kutoka kwenye Baraza la Kata na Baraza la Kata halifanyi kazi. Sasa huyu mnayemwapisha maana yake ni nini? *How do you justify existence* ya vitu hivi? Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba wa Wilaya kazi yake ni nini kwa sababu hapokei mashauri yoyote kwa sababu Baraza la hapa katikati kama ilivyokuwa Mahakama ya Mwanzo halipo na mashauri haya hayapelekwi kwenye Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mabaraza ya Wilaya katika maeneo mengi tu ambayo kuna matatizo ya ardhi, lakini fedha wanazopewa ni kidogo sana na ndiyo maana mimi nasema kwamba kati ya 1992 na leo kuna mashauri zaidi ya 100 yamekwama Wilayani. Kinachotokea ni kwamba, fedha zikija wanafanya kazi kwa muda wa wiki mbili baadaye wanarejea makwao na inaonekana wanaketi kama mara nne kwa mwaka. Kwa hiyo, mashauri mengi yamekaa na haki za watu, watu wamenyanyasika sana.

Kinachotokea sasa hivi ni kwamba, kwa ajili ya hali hii ya kisheria watu wametambua kwamba ukimdhulumu mwenzako kwa sababu hamna shauri litakaloendelea, unaweza ukamnyanyasa mwenzako kwa miaka mingi tu na haya yote yameletwa na Sheria ya Ardhi bila ya kujua kwamba masuala haya yanataka fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Baraza la Mkoa, mimi nina bahati sasa hivi nina *cause list* ya *Customary Land Appeals Tribunal* ya Arusha na Manyara. *Cause list* ya siku moja tu ya tarehe 24 Mei, ina mashauri ya kuanzia mwaka wa 1992. Hii maana yake ni kwamba, kama mtu amesimamishiwa ardhi yake mpaka leo hatujui anakula nini na labda nitaje hili ni shauri limetokea Wilaya ya Arumeru. Shauri namba 4 la mwaka 1992 kati ya Lorivina Nicholaus dhidi ya Charles Muruo, hili shauri ni toka 1992 na linahusu shamba na hii yote ni mlolongo wa ucheleweshaji kwa sababu ya hawa watu kuwepo tu kwa majina kama ninavyotaja hapo juu, hawana kazi wanayofanya kwa sababu hakuna fedha. Kesi kama hizi ni nyingi, kwa Wilaya ambayo mimi natoka nimesema ni zaidi ya 100 na mbele yangu hapa katika hii *cause list* ya tarehe 24 Mei hadi tarehe 16 Juni katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Arusha ambalo ni kwa ajili ya Arusha na Manyara, ni mashauri zaidi ya 70. Hii ni *cause list* ya siku moja na ni kusikilizwa siyo kuzitolea hukumu na kusikiliza, maana yake ni pamoja na Mawakili kuwepo na mjadala wa muda mrefu.

Sasa ninachotaka kusema hapa ni kwamba hivi tufanye nini? Ili kuwepo na uhalali wa majina haya na viapo hivi, Waziri ni lazima aje na bajeti kamilifu ya kuendesha Mabaraza haya kwa ngazi ya Kijiji, ngazi ya Kata na ngazi ya Wilaya. Kwa Mkoa hatuna tatizo kubwa naona kwamba wanafanya kazi nzuri isipokuwa rufaa ni nyingi. Idara ya Ardhi ya Mahakama Makuu haina tatizo kwa sababu Jaji yupo na analipwa vizuri, lakini nadhani baadaye atakuwa *redundant,* hatapata rufaa kutoka ngazi ya chini kwa sababu hamna vyombo vinavyofanya kazi ngazi ya chini. Hili ninalielekeza zaidi kwa Waziri wa Ardhi ili atuletee bajeti ya kukidhi Mabaraza haya ili kutatua migogoro hii ambayo inatusumbua sana katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili ni hili la sheria ya mwaka wa 1999 la Mashirika ya nje na Balozi za Nje kumiliki ardhi. Hakuna tatizo. Tatizo ni masharti gani watapewa na kutoa masharti ni kitu kimoja, lakini kusimamia masharti ni jambo lingine kabisa. Kuna ushahidi wa kutosheleza kwamba Mabalozi sasa hivi wanakodisha ardhi, wanakodisha majengo, majengo mengine yanakuwa ya baa, watu wanapigana humo na ushahidi upo. Kuna maeneo yanayomilikiwa na kufanyiwa biashara na Mabalozi wa nchi za kigeni. Wanakodisha kwa watu kwa bei kubwa, makontena makubwa yanahifadhiwa kwenye maeneo kama haya. Masharti haya maana yake ni nini kama hayatekelezwi na chombo chochote?

Mtu anaweza kukataa kutii sheria kwa sababu ya tukio kutokea katika maeneo ambayo siyo sehemu ya Tanzania. Sasa ulegevu wa namna ya kusimamia masharti tuliyonayo utachukuliwa hatua gani? Masharti haya yatakuwa na maana gani kama hamna anaeyasimamia?

Mheshimiwa Spika, kwa vile nilisema kwamba nitaongelea maeneo mawili tu katika Muswada huu wa mabadiliko ya sheria mbalimbali, napenda kumalizia kwa kusema tu kwamba, sitarajii majibu yatapatikana hapa leo. Majibu yatapatikana kwa eneo nililosemea katika Bajeti ya Waziri wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kuishukuru Serikali kupitia kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuleta marekebisho haya. Nitachangia maeneo mawili tu, eneo la Muswada ule wa *SUMATRA* au udhibiti wa usafiri na usafirishaji nchini, halafu na Muswada wa Sekta ya Chai. Sheria hii ya *SUMATRA* ilitungwa muda uliopita na haijatumika. Kwa hiyo, kuleta marekebisho haya ni jambo muhimu sana ili sheria hiyo iweze kutumika kwa sababu sasa hivi kuna mwanya hapo, watu huenda wanahangaika kuhusu nani anadhibiti nini na kadhalika. Kwa hiyo, naunga mkono na pengine Muswada huo wa marekebisho ukipita tumwombe Mheshimiwa Rais naye aupe kipaumbele kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ambao wanashughulikia baadhi ya Mashirika wanaulizwa hii *vacuum* au *gap* hii inakuwakuwaje?

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kusisitiza hapa ni kwamba, kuna Shirika lililopo, hili la *Tanzania Central Freight Bureau* la kudhibiti shehena, ningeshauri Serikali ifanye maandalizi mapema kabisa ili wale Wafanyakazi ambao hawatachukuliwa na *SUMATRA* kwa kweli walipwe malipo yao kabla ya kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kuhangaika kwingi sasa hivi kwa baadhi ya Wafanyakazi kwa sababu utakuta si tatizo la Serikali, lakini vyombo hivi vimekata mafao ya Wafanyakazi na havikupeleka kwenye Mashirika yanayohusika kama *PPF* na *NSSF.*

Kwa hiyo, utakuta hapa wanahangaika siyo kwa sababu Serikali imeshindwa kuwalipa, lakini kwa sababu hao waliokata mafao yao hawakupeleka kule yanakotakiwa.

Nadhani kwa sababu hii inajulikana waziwazi kabisa jambo hili lingeshughulikiwa sasa kwamba Mashirika hayo hasa hili ambalo sasa baadhi ya Wafanyakazi huenda hawatachukuliwa na *SUMATRA,* basi mafao hayo yahakikishwe kwamba yamefika kule yanakotakiwa na kama hayatakuwa yamefika basi Serikali yenyewe itafute njia ya kuyafikisha ili kabla hawajaondoka hawa wawe wamelipwa ili tuanze *chapter* mpya. Hayo ya nyuma tuyaache, lakini tuanze *chapter* mpya maana sasa hivi tuna masuala ambayo yanaletwa mbele ya Kamati za Bunge ya wafanyakazi wa Mashirika ambayo yamebinafsishwa ambao hawajalipwa mafao yao.

Jambo la pili, katika hoja hii ya *SUMATRA* napenda kuipongeza sana Serikali na hasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka kinga. *Order* za kukamata mali zimeleta athari nyingi sana katika baadhi ya maeneo na nimeshangaa sana watu wa Upinzani wanasema kuweka kinga ni kukaa juu ya sheria au kukaa juu ya Mahakama. Si kweli, kwa sababu kinachofanywa hapa ni kuweka kinga na kinga hii ni muhimu. Kwa mfano, *SUMATRA* itakuwa na magari, itakuwa na majengo ya kufanyia kazi ya kudhibiti usafiri na usafirishaji, sasa unapoyakamata haya na kuzuia maana yake ni kwamba umezuia huduma zisifanyike. Hiyo ndiyo mantiki yake, usizuie kitu ambacho kitaathiri huduma za vyombo vingine. Sasa hii ya malipo nadhani ndiyo mbadala wake kwamba kama kuna kiasi kinacholingana na hiyo thamani ya mali inayoshikwa, basi hicho kiwango kilipwe. Ina maana kwamba, sasa Mahakama itoe hiyo *alternative order,* siyo *order* ya kukamata kitu ambacho kitazuia utoaji wa huduma, ndiyo maana yake hasa mimi nilivyoielewa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono kabisa hatua hii kwa sababu hatua hii kwa kweli inaweka utulivu katika utoaji wa huduma na wala haipingani na *order* za Mahakama. Isipokuwa *alternative* ya kuzuia mali za kutolea huduma au gari linataka kwenda bandarini kwenda kucheki meli unalizuia, ina maana meli haitachekiwa, nadhani hiyo ndiyo mantiki ambayo imefanya iwepo kinga. Kwa hiyo, nashukuru sana marekebisho hayo yazidi kukamilishwa ili sheria hiyo iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ninalotaka kuchangia ni kuhusu Sheria ya Sekta ya Chai. Nakubaliana sana na mapendekezo haya ya kurekebisha muundo wa bodi ili kuondoa utata ambao upo. Nasema hivyo ku-*declare interest* yangu. Mimi ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kwa sababu niko katika Bodi ya Chai. Kuna utata wa wazi kabisa kwa hiyo, utaondoka. Isipokuwa nina ushauri kidogo kuhusu kuteua Naibu Mwenyekiti, kila mwaka, *continuity* pale kidogo inakuwa na matatizo. Mimi ningependekeza kwamba, kwa sababu kipindi cha Bodi ni miaka mitatu, kwa hiyo, baada ya mwaka mmoja na nusu basi achaguliwe mwingine ili iwe na Naibu wawili katika kipindi hiki cha miaka mitatu. Hiki kipindi cha mwaka mmoja kwa kweli hakina *continuity* ya kutosha hata sisi wenyewe katika Kamati za Bunge, wakati zilikuwa zinateuliwa kila mwaka utakuta hakuna kuzamia sana kwenye shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho ningependa kukigusia hapa, kwa wale wenzetu ambao pengine hii sekta ya chai haiko katika maeneo yao, katika maeneo yetu ya chai tuna wakulima wa namna mbili. Tuna wakulima wakubwa wa ma-*estate* makubwa tu, halafu tuna wakulima wadogo wadogo. Sasa wakulima wadogo wadogo hawa wamepata faraja wakati Serikali, ilipounda Wakala wa Chai. Kwa sababu Wakala wa Chai ilisaidia kuwaunganisha hawa nguvu zao kwa pamoja mpaka baadhi wameweza kuuziwa viwanda vya kuchambua chai. Sasa hivi kuna vuguvugu na shinikizo la kutaka kuua Wakala wa Chai, iliyotokana kwa wakulima wakubwa hawataki sisi wakulima wadogo tujue soko lina-*behave* vipi huko nje. Chombo ambacho kinasaidia wakulima wadogo yaani Wakala wa Chai, ukikiondoa ni kwamba hawa wakulima wakubwa ndiyo watakamata hiyo sekta, hilo lazima lieleweke hivi kiuchumi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wakala wa Chai kwa kweli ni muhimu katika kuendeleza chai kupitia kwa wakulima wadogo. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na Serikali, tuwe makini sana hapo katika suala hili. Wakulima wakubwa wamesema waziwazi kwamba, Wakala wa Chai ni *useless thing, we don't need it*. Lakini sisi Wakulima wadogo tunataka Wakala wa Chai kwa kweli. Kwa sababu hata hivyo majukumu ya hizi taasisi mbili ni tofauti: Bodi ya Chai kazi yake ni kudhibiti na kuweka *standards,* Wakala wa Chai ni kusaidia wakulima wadogo hawa, wawaelekeze namna ya kupata misaada kutoka wapi, wanawaelekeza namna ya kuongoza sekta hii. Wanawaelekeza Wakulima namna ya kutumia nguvu zao kuingia vizuri katika kilimo cha chai.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nasema tena naunga mkono kabisa marekebisho haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii. Kabla sijaendelea kuchangia hoja, ningependa nami nichukue fursa hii kumpongeza sana ndugu yetu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wa kishindo alioupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii ya mabadiliko ya sheria kuna masuala mawili makubwa ambayo ningependa kuzungumzia. Moja ni kuhusu suala la sheria hii ya chai pamoja na ya mkonge. Ninashukuru kwamba mabadiliko haya yameletwa lakini ningependa kuzungumzia masuala mawili. Moja ninavyoelewa mimi na bahati nzuri nina-*declare interest* na mimi ni Mjumbe katika Bodi ya Mkonge kuna mapendekezo mengi sana yalikuwa yamependekezwa, lakini matokeo ni kwamba, kuna eneo hili moja tu la Bodi ya Wakurugenzi ambalo limezungumziwa. Sasa sijui hayo mengine yamekuwaje. Pili, katika suala hilo ni kwamba, zimezungumziwa bodi mbili, sasa sijui bodi nyingine zitaendelea vile vile au hazihitaji mabadiliko. Lakini tatu ambalo limenifanya nipate kutoelewa ni kwamba, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, alipoleta mabadiliko haya alielezea haya kwamba haya mabadiliko yanafanywa ili kuwapa wenyewe fursa zaidi. Sasa hii wenyewe mimi sikuelewa wenyewe ni nani maana *stakeholders* ni wengi na hao wenyewe wanaozungumziwa ni nani? Pengine ufafanuzi huo ungenisaidia Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni hili la Sheria ya Ardhi. Kwenye ardhi kumekuwa na matatizo mengi na sheria ile ambayo tuliipitisha hapo awali ilikuwa na madhumuni ya kutupunguzia na kuondoa matatizo hayo. Moja ya matatizo ambayo tulihisi pengine yangeweza kujitokeza ni fursa nzuri ambayo wamepewa wananchi kwamba, wanaweza kutumia ardhi kama dhamana. Lakini wakati tukizungumza sheria hii vile vile tulitoa maoni kwamba ni vizuri tukawa na tahadhari nzuri pale tunapoweka ardhi yetu kama dhamana. Kwa sababu kuna wafanyabiashara na hasa wakopeshaji na mabenki mbalimbali na asasi nyingine za nje ambazo zingeweza kuchukua fursa hii zikafanya ujanja ujanga na hatimaye ardhi ile ibaki huko huko kwao.

Sasa zaidi ya hapo tuliongeza swali hili kwamba, wawekezaji katika maeneo yale ambayo yameainishwa pamoja na taasisi za kigeni zinaweza zikatoa ardhi kwa kumiliki. Sasa hilo linanitia wasiwasi. Baadhi ya wasiwasi umeelezwa na wenzangu. Lakini pengine ni vizuri ningepata ufafanuzi hili limeletelezwa na nini? Tahadhari zile ambazo tuliziona awali zimetoweka au tahadhari mpya zinawekwa ili kuhakikisha kwamba ardhi yetu ambayo ni raslimali muhimu sana haichukuliwi kienyeji, kiujanja ujanja hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nashukuru sana kwa kupata nafasi siku ya kwanza ya Bunge lako Tukufu. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa na wananchi wa jimbo lake kuwa Mbunge kwa kura nyingi. *(Makofi)*

Pia vile vile nitoe rambirambi zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lushoto kwa Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuleta mabadiliko katika sheria mbalimbali. Pengine nitoe masikitiko yangu kwamba, sheria nyingine tunazibadilisha hata kabla hazijatumika. Hii ni aibu na Serikali ikubali kwamba ni kosa kubwa kutunga sheria unaifanyia mabadiliko kabla hujaitumia. Sasa hapo utakapoitumia itakuwaje? Kwa hiyo, *SUMATRA* ni mfano mzuri wa sheria ambayo haijatumika, *EWURA* ni mfano mzuri wa sheria ambayo imekwishatungwa na Bunge limepitisha, Rais amesaini lakini haijatumika. Leo liko tatizo kubwa la mafuta kupanda bei wala hakuna mdhibiti kwa sababu *EWURA* haijaanza kutumika. *(Makofi)*

Sasa nirudi katika Muswada, nitazungumzia maeneo matatu la kwanza ni la *SUMATRA*, la pili nitazungumzia ardhi hasa katika upande wa Mabaraza. Lakini nianze na *SUMATRA.*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, mwaka 2003 ilinipa nafasi ya kuhudhuria kikao cha Umoja wa Mataifa katika eneo la Usafiri wa Meli Duniani *(International Maritime Organization).* Nilipata bahati kuhudhuria kikao kile ambacho kwa kweli nilijielimisha sana. Kwa bahati nzuri wakati

nimekwenda kule tulikuwa tumekwishapitisha sheria ya *Merchants Shipping Act* ambayo hii sheria ndiyo inayofanya nchi kutambulika Kimataifa. Kwa bahati nzuri mambo yaliyozungumzwa na suala ambalo leo tunalipitishia mabadiliko linahusiana pia na utekelezaji wa sheria hiyo. Hili linahusiana na suala la usalama wa meli *(Maritime Safety and Security).* Hili linatambuliwa na Umoja wa Mataifa na nchi yetu imepata bahati kukubaliwa kwa sababu tulikwishaunda na tulikwishapitisha Sheria ya *Merchants Act.* Sasa linalotokea leo ni utekelezaji wa sheria ile. Labda mimi nitoe tahadhari tu kwamba, utekelezaji wa *Marine Service Safety* ni kitu muhimu sana. Lakini liko tatizo ambalo litajitokeza katika nchi yetu kwa sababu kwa sasa hivi tunatekeleza makubaliano katika *conversations* za Kimataifa. *Conversations* za Kimataifa zinaitambua Tanzania kama nchi moja.

Mheshimiwa Spika, tulipopitisha Sheria ya *Merchants Shipping Act* ililetewa mabadiliko hapa hapa Bungeni kwamba sheria ile itatumika kwa Tanzania Bara haitatumika kwa Tanzania Visiwani. Sasa linalotokea pamoja na kwamba tunafanya mabadiliko haya ya usalama wa meli *(Marine Safety and Security),* yanatambuliwa Kimataifa. Lakini kuyatekeleza mabadiliko haya kwa kutambuliwa Tanzania Bara tu, Tanzania Visiwani (Zanzibar) isipotambuliwa, ina maana hata ile *Merchants Shipping Act* na wenzetu katika *International Maritime Organization* wanaweza wakatufuta kama Taifa na tutaonekana waongo Kimataifa.

Sasa hili nalitoa kama tahadhari kwamba, Serikali iendelee kuchukua juhudi, ni ukweli kwamba tunafanya mabadiliko mazuri ili tutambulike Kimataifa. Lakini kama sheria zetu hazijakamilika basi tutaonekana sisi ni walaghai. Maana tunawaambia kule tuna sheria, lakini sheria hiyo, inatafsiriwa katika sehemu moja ya nchi na wao hawatutambui kama sehemu moja ya nchi, wanatutambua kama Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Hili nalitoa kama tahadhari kwamba, juhudi ziendelee kufanyika vinginevyo tutafika mahali meli hazitaruhusiwa kuweka nanga Zanzibar na sisi hatutambuliwi katika Umoja wa Mataifa kwa sababu sheria yetu haiku-*cover* maeneo ya nchi nzima. Meli haiwezi ikaja na mzigo Dar es Salaam ikashindwa kushusha Zanzibar au italeta matatizo sana katika utekelezaji wa sheria za Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe tahadhari hiyo tu na pia kuiomba Serikali kwamba katika bajeti kutekeleza hizi *conversations* hizi ni ghali kwa hiyo, inawezekana *TCFB* na hasa hii *SUMATRA* ambayo inapelekwa huko, inaweza ikashindwa kifedha. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikatambua hilo na ikatenga hela za kutosha ili hii *SUMATRA* iwe na uwezo wa kutekeleza Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningependa kuzungumzia nisingependa nilirudie sana, lakini ni vizuri kama likitajwa na Wabunge wawili/watatu, linakuwa na uzito. Suala hili la Mabaraza ya Ardhi, Mheshimiwa Philip Marmo, amelitaja vizuri na bahati nzuri amelieleza kwa undani. Sisi tunaotoka katika maeneo ambayo yana uhaba wa ardhi tatizo hili ni kubwa. Sheria ya Ardhi sasa hivi imesimama haitekelezeki. Mabaraza haya hayapo, hayafanyi kazi, kwa hiyo migogoro ni mikubwa sana kule vijijini.

Sasa tunaomba kwa kweli Wizara ya Ardhi, ichukue hatua za makusudi kutatua haya Mabaraza yafanye kazi kwa wakati kwa sababu wananchi kunapokuwa na kesi ambazo zinapaswa kuamuliwa ina maana ya kwamba, shughuli zote zinasimama katika mashamba yale ambayo yana migogoro. Kwa hiyo, mashamba yale yamekuwa mapori, wananchi hawaelewi wafanye nini, bado sheria inatamka kwamba, haijaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ilichukue suala hili kwa msingi na msimamo mkubwa ambao utalifanya lifanikiwe mapema zaidi. *(Makofi)*

La tatu, katika hilo ni suala ambalo leo tumeletewa katika marekebisho ya sheria na limekuja katika karatasi hili na maelezo yaliyoko humu ndani mimi ninayahofu kidogo. Suala hili la kutoa kibali kwa *NGOs* kupewa umiliki wa ardhi. Ni kweli ilivyoelezwa hapa na ukienda ukurasa unaofuata inasema kwamba, Waziri atakuwa na mamlaka ya ku-*revoke* na pia vifungu vya 47,48 na 49 vitatumika pamoja na mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nina woga sana wa sheria zinazotamka bila kutoa utaratibu wa kutekeleza mara moja ukapelekwa katika sheria nyingine. Upo ushahidi wa kutosha kwamba, *NGOs* au mashirika yanaambiwa siyo ya Kiserikali yamepewa ardhi na ardhi imetumika visivyo na wamezitumia ardhi kinyume cha makubaliano. Mimi jimboni kwangu kule nina ushahidi wananchi wale wale walionyang'anywa ardhi yao wanakodishwa ardhi ile. Lakini kwa sababu huyu aliyeipata ardhi hii alitamka kwamba atatoa huduma hizi na hizi hazitoi. Leo anageuka anawakodisha wananchi wale wale waliotoa ardhi yao. Kwa kweli Serikali inakuwa katika hali mbaya sana. *(Makofi)*

Mimi nina mfano mzuri sana wa Kijiji cha Ubili, wametoa ardhi kwa nia nzuri wajengewe shule, wajengewe *dispensary,* yule aliyepewa ardhi ile hafanyi hayo, kinyume chake anawakodisha wananchi ardhi ile na ushahidi upo. Sasa Waziri sijui ataniambiaje kama huyu ni mmoja na najua wako wengine wengi ambao Wabunge wakiulizwa hapa watasema. Sasa leo tunaendelea ku-*liberalize* bila kuimarisha *regulation*, ku-*regulate,* maana tatizo la nchi yetu ni kutunga sheria bila kuweka utaratibu mzuri wa kuitekeleza sheria, hatimaye watu wanachukua nafasi hii ya udhaifu wetu kujinufaisha.

Hii iko katika maeneo mengi na haya ninayozungumza kama nilivyosema mwanzoni, kwa mfano, *EWURA* haipo, ku-*liberalize* eneo la mafuta ni sahihi maana tunakwenda na utandawazi hata tukikataa wataleta. Lakini bila kujiwekea taratibu za udhibiti ni kama unafungua mlango mbu, nyoka, wataingia watakuuma katika nyumba yako. Sasa mimi ndiyo hofu yangu kwamba ni vizuri tunapolegeza masharti basi tuwe katika sheria hizi, tuna taratibu za kudhibiti na kuhakikisha kwamba yale tuliyoyaweka kweli ndiyo yanayotekelezwa. Lakini udhaifu uko mkubwa kama nilivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuunga mkono hoja kwa tahadhari hii tu ya ku-*liberalize* eneo la ardhi bila kuwa na uhakika kwamba likitokea tatizo tutalirekebisha vipi. Kwa hiyo, ningependa sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, aje atuambie kwamba katika sheria hii hivi vifungu alivyosema vya 47,48 na 49 ambavyo mimi sina hapa, je, vitatusaidia kuwadhibiti hawa?

Kuna *process* gani ambayo Waziri kwa haraka sana atachukua hatua ku-*reprocess* ardhi ambayo kwa kweli haitumiki kwa makusudi yaliyokusudiwa. Hilo ndiyo Wabunge, wangelitaka ili tumwajibishe Waziri haraka sana kwamba katika sheria hii ulipaswa huyu alitamka hivi, tunaomba ardhi irejeshwe.

Sasa sioni mahali panapotamkwa, labda Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atusaidie kama kweli hapo kwa niaba ya wananchi tutakubali kwa shangwe kwa sababu hakuna njia nyingine, hawa ni *partners* wetu katika *development* lakini siyo wote wanakuja kwa nia nzuri, wengine kwa kweli wanakuja kwa nia mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya hayo nitaunga mkono hoja, baada ya kupata maelezo hayo kutoka kwa Waziri na wanaohusika. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumzia marekebisho mbalimbali ya sheria. Lakini kwangu napenda kuhusika zaidi na chombo cha *SUMATRA.* Niungane basi na wenzangu waliompongeza *comrade* mmoja, anaitwa Mheshimiwa Danhi Makanga. *Comrade* ameshinda vizuri sana, tunampongeza kweli kweli kwa sababu moja tu, pamoja na sababu zingine zote kwamba si jambo la kawaida sana kwa Mwenyekiti wa Chama cha Kitaifa, anagombea Urais, anashindwa katika uchaguzi, badala ya kubaki kule juu anakwenda kwenye jimbo, huyu ana matatizo makubwa sana! *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, kwa kusema kweli tunapompongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, tumpongeze katika sura hiyo kwamba amemshinda mtu ambaye amegombea Uraia. Haijapata kutokea. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Haijawahi kutokea. *(Kicheko)*

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwape pole sana, rafiki yangu, Mheshimiwa Abdallah Kigoda kwa msiba uliompata yeye mwenyewe na dada yake ambaye ni Mbunge mwenzetu hapa, kwa kweli ni jambo ambalo limetusikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, chombo hiki cha *SUMATRA* kimerithi baadhi ya kazi ambazo zimetoka kwenye chombo kinachoitwa *Tanzania Central Freight Bureau.* Chombo kile kwa habari ambazo ninazo ni kwamba, *Tanzania Central Freight Bureau* toka imeanzishwa mara zote imekuwa ikipeleka faida Hazina. Hata mara moja hakijapata hasara chombo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo chombo ambacho sasa kazi zake zinachukuliwa na *SUMATRA.* Nasema hivyo kwa sababu vyombo hivi tunavyoviunda tuviunde kwa nia nzuri tu, lakini lazima tuifuate mifano ya maeneo mengine ambayo sasa majukumu yake yamekuja kwake. Wafanyakazi wa *Tanzania Central Freight Bureau* wako wachache sana lakini wameweza kufanya kazi yao vizuri kweli kweli na hakuna ubabaishaji, vizuri sana. Sasa hapa nimefarijika kwa jambo moja tu kwamba, imeamuliwa sasa kwamba wafanyakazi wa chombo hiki watahamishiwa kwenye chombo kipya cha *SUMATRA.*

Wasiwasi wangu ni kwamba, tumekuwa na matatizo na viwanda vyetu na mashirika yetu ambayo kwa sheria tumepata nafasi ya kuwapa watu binafsi na bahati nzuri *SUMATRA* itabaki Serikalini. Lakini mara zote tumekuwa na shida na wafanyakazi kuwalipa maslahi yao, mpaka hivi sasa kuna baadhi ya viwanda katika Mkoa wa Morogoro, wafanyakazi mpaka leo hawajalipwa masilahi yao. *(Makofi)*

Sasa napenda kusema kwamba, si vibaya hata kidogo kwa chombo ambacho kimefanya kazi nzuri kama *Tanzania Central Freight Bureau,* wafanyakazi sasa wanaambiwa watachukuliwa na chombo kipya, uamuzi huu ni uamuzi mzuri sana na ni uamuzi wa busara. *(Makofi)*

Ombi langu ni kwamba, sidhani kama itakuwa ni sahihi, nadhani ni vizuri zaidi kama wafanyakazi hawa watalipwa mafao yao kabla hawajakwenda kwenye chombo cha *SUMATRA*. Kama watachukuliwa kwenye chombo kipya basi waende wafanyakazi ambao ni *clean,* hawana malalamiko na walikotoka. Sasa naomba sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye amewasilisha Muswada huu pamoja na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, naomba kusema baadaye watusaidie.

Ninashauri kwamba wafanyakazi hawa walipwe maslahi yao kabla hawajakwenda kwenye chombo kipya kuepuka kero, kuepuka matatizo, kwa watu ambao wamefanya kazi yao vizuri haipendezi hata kidogo kuendelea kujibu maswali kwa wafanyakazi ambao wamefanya kazi yao vizuri na sasa wamefanikisha na kimeundwa chombo kipya wao bado wabaki na matatizo.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni kwamba, nimepata moyo sana kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ameleta marekebisho hayo pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa wakati muafaka kabla ya bajeti ya Wizara kwa sababu tunapitisha chombo hicho na ameamua sasa kukiunda kabla ya bajeti yake. Naspenda kusema kweli Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ametumia busara sana kwa sababu tulikuwa tumejiandaa kumwuliza kwamba tumepitisha *SUMATRA* iko wapi? Kwa hapa naona huyu *comrade* mmoja, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, anafanya maandalizi. Hawa mimi ndiyo ninawaita Ma-*comrade,* wengine wote ni ndugu tu. Amefanya maandalizi ya kisayansi kabisa kwamba kabla ya bajeti yangu nihakikishe kwamba chombo hiki kimeundwa. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa kuona mbali. Hivyo ndivyo tunavyotaka iwe, tufanye maamuzi tupitishe sheria ambayo mara moja mwenzetu anayehusika atatekeleza. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa kwa sababu ya hali yenyewe ilivyokuwa nzuri, nimeamua kusimama kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa uharaka na nimejifunza tu kwamba, hata vyombo vingi sana vilivyoko chini yake, tabia yake ni hiyo hiyo ya kuhakikisha vyombo vinakwenda vizuri. Nadhani Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ungeendelea na tabia hii kwa sababu inatuthibitishia kwamba kwa kweli wewe ni askari wa mwavuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kusema tu kwamba, ninakubali kwa dhati kabisa marekebisho yote ambayo yamefanywa katika kuweka sawa chombo cha *SUMATRA.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kushukuru kwa dhati kabisa kwa kupata nafasi siku ya leo tarehe 8 Juni, 2004, ni siku yenye historia nyingi tu. Ni siku ambayo watu ambao walikuwa *sensitive* na *sensible* walikutana wakataka kushindana. Mtu ukiwa *sensitive* utakuwa na *power* ya ku-*feel,* kufikiria mwelekeo, ukiwa *sensible* una-*feel* na ku-*reason.* Marekebisho haya yana *reason* zake kwa sababu aidha sheria inaweza ikatungwa baadaye ukiona bado kuna matatizo ya kiutekelezaji au migongano katika sheria na sheria au vifungu vyenyewe kwa vyenyewe vinakuwa vinaleta matatizo kwa *league framework,* basi unaleta marekebisho na warekebishaji ni sisi hapa, huwezi ukafanya mambo hayo peke yako, ninyi mnafanya kanuni tu. Kwa hiyo, umepeleka mahali pake. Huyu ni *goalkeeper* mzuri unadaka mpira unarudisha uwanjani. Ninashukuru sana kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *SUMATRA,* Mheshimiwa *Comrade* Kasapira, amezungumza mengi na ukweli ni kwamba sasa iende ikafanye kazi. Tunaipa baraka ikafanye kazi ili angalau migogoro midogo midogo inayojitokeza, wale ambao hawana pa kukimbilia, sasa wana maeneo ya kwenda. Kwa hiyo, tunatoa ruksa hiyo waende wakafanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Lingine ni kwamba, kwanza nilitaka kupongeza siyo kurudia lakini kuna upongezaji wa aina yake. Mheshimiwa Danhi Makanga, umeshinda kwa sababu *value* ni ndogo waliku-*underlet.* Kuna siku moja Maprofesa Duniani waliambiwa waende kujibu swali katika Chuo Kikuu cha kule *Q London,* waliambiwa wajibu swali moja tu, waliambiwa Maprofesa wote wajiandae atakayeshinda atapata zawadi nono. Basi Maprofesa wengi wakasoma ma-*book* yao mengi sana. Sasa wakajiandaa walikuwa karibu 200 hivi walikwenda kule Chuo cha Lasgo kujiandaa kujibu swali hilo. Waliulizwa swali waliambiwa mapema kwamba, je, useme neno la kwanza la duniani la mtu ambaye amelitamka, basi Maprofesa wakajiandaa wakasema hewa wengine mama, wengine bibi, kumbe bahati mbaya sasa waliojiandaa walishindwa. Kulikuwa na mama mmoja bahati nzuri chumba cha *labour* kilikuwa karibu alijifungua mtoto akasema ng'aa! Ndiyo kashinda huyo huyo wakasema mwite huyo. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, huwezi ukajiandaa kwa ushindi wakati mwingine kumbe kuna watoto watachukua madaraka hapo hapo mbele yako, pamoja na kuwa ulijiandaa kwa muda mwingi. Kwa hiyo, maandalizi wakati mwingine yana matatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nakwenda kwenye *Food, Drugs and Cosmetics,* kuna kipengele kwenye sheria ya *Food, Drugs and Cosmetics* na nimesimama kuzungumzia eneo hilo ambalo ni muhimu sana kwa sababu Watanzania hakuna Mtanzania asiyevuta hewa, asiyejipodoa, asiyetumia kitu chochote ambacho ni cha chakula siyo kula, Watanzania wote wanakula, sheria hii inahusu watu wa aina hiyo, Tanzania nzima nao wanahisia. Kwa hiyo, sheria

ya chakula madawa na manukato upo umuhimu wa kurekebisha mara kwa mara kwa sababu tunakokwenda chini ya mfumo huria, wapo wenzetu ambao wenye tabia mbovu ya kupenda madaraka, wenye uroho wa kuleta vitu ambavyo ni vibovu katika nchi hii ili wapate matatizo. Ndiyo maana nimesema ingawa nchi hii wapo wastaarabu lakini wapo wachache waroho. Katika mgao wa mambo wao hawatumii vijiko vya kawaida, wanatumia kujilisha kwa mabeleshi. *(Kicheko)*

Sasa hao sheria hii itawabana. Hata kipindi cha njaa, wakati ambapo dawa zimepotea wanaleta madawa ambayo pengine yame-*expire* kwa hiyo, sheria hii itawathibiti katika kuhakikisha kwamba, *Food, Drugs and Cosmetics* wanapewa vifaa vilivyokuwa na *quality* nzuri ili Watanzania wapone na wafanye kazi vizuri wazalishe mali, wazalishe vyakula vyao, waweze kula vyakula *fresh* badala ya kutegemea mchele wa *VIP,* ambao wanajivunia Wizara ya Kilimo na Chakula wakati wa njaa badala tuzalishe wenyewe tuendelee vizuri. Kwa hii sheria ni nzuri.

**MBUNGE FULANI:** Tunategemea mchele wa Kyela.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Tunategemea wa Kyela, ndiyo sawa sawa mama kaniunga mkono hapa.

Mheshimiwa Spika, kuna kipengele kimoja kilikuwa kinanipa wasiwasi, vitu vinaitwa dawa. Kwa mfano, kama tulitakiwa *detergent* kama sabuni ambazo zina aina ya vipodozi lakini vile vile hutumika kama ni dawa katika kupanga lile jedwali letu. Hapa kuna dawa hizi za *whitedent* ambazo ni dawa fulani ambazo zinawekwa kwenye mswaki halafu mswaki huo huo huenda kwenye kusugua meno ili yawe meupi. Sasa hiyo kama dawa, kuna kama *Aha, Whitedent,* naona matangazo akiona “mimi ni mama yenu nimevaa koti jipya, mimi ni nani”. Sasa baada ya kuvaa koti amebadilika jina tena tunaambiwa wewe ni mama yetu pamoja na kuvaa koti jipya. *(Kicheko)*

Lingine madawa kwenye maduka majina yaanza kuibukaibuka pamoja na kwamba *chroloquine* tumeifuta tulikuwa tunategemea *SP* na dawa zingine. Wakati huo tulikuwa na *Qwinorine, unhydride compounds, Vitamin B Complex, Sambex,* ambayo inatokana na *Chloroquine.* Ni aina zote za *Chloroquine, Malaraquine, Zainabuqine, Amidiaquine, Pawaquine* zilikuwa zote zimefutwa. Nashukuru sana kwa Wizara kuchukua hatua hii. Kwa kweli dawa hizi kwenye maduka sasa hivi hazipo, pamoja na kubadilisha majina na kuweka *trade names.* Lakini Sheria hii na huruma hii ya Wizara yenyewe ya Afya wameisimamia vizuri madawa haya hayapo.

Sasa hivi kumeibuka nyingine inaitwa *Malafia* na kuna majina mapya mengine ambayo naorodhesha nitaeleza wakati nitakapochangia Wizara ya Afya. Sasa yale wayaangalie watumie Kitengo chao ili kuangalia kama *Quinorine Restructure* katika hiyo au vile vile wasije wakawa mamebadilisha majina yale yale ili kubadilisha jina lakini *composition* ikawa ile ambayo imekatazwa katika mfumo wa Sheria ile.

Hapa kuna majina kama *Vitamin B Complex, common name* wanaita *Starndex* kuna watu wanaandika kisheria wanaita nguvu moja au kimatu. Sasa majina kama yale

yapigwe marufuku kwa sababu haiwezi kumridhisha mgonjwa, bali anajua basi ni dawa ya kupenda kula tu, kumbe wakati mwingine ni dawa ambayo inasaidia mambo mengine mengi. Kwa hiyo, majina yale vile vile yadhibitiwe katika Baraza ambalo linaundwa ili kusudi tusiwapotoshe Watanzania katika kusoma majina ya madawa haya. Kwa sababu watu wanapenda majina, wanapouza kitu kwa jina zuri kama ukisema kama kwa mfano, ukitangaza hapa, ukitangaza hapa ukisimama, unasema mimi nauza nyanya zilizopondekapondeka na zimeoza. Hawezi kununua mtu.

Lakini ukisema nauza masalo safi, watu wanachukua. Lakini ni ile ile ustaarabu wa lugha tu au mtu unasema mimi nauza maziwa yaliyochacha ambayo yameharibika, ama yameganda hanunui mtu lakini kama unaweza ukasema mtindi *fresh,* watu wananunua. Sasa kwa utaratibu huo, wafanya biashara, wanaweza wakautumia ili kusudi waweze kuwavuta Watanzania wakaanza kununua, lakini Wizara ya Afya, nashukuru mmesimamia haya na mmeunda Kamati mbalimbali ambayo inasimamia. *(Makofi/Kicheko)*

Hatua ya pili nasemea kuhusu ardhi. Kesi ni nyingi napenda hapa nimpongeze Mkuu wa Wilaya ya Morogoro na Mvomero wana utaratibu mzuri sana. Asubuhi niliwagonga kuhusu ugawaji wa vyakula, fuatilieni huko, Tarafa ya Ngerengere na maeneo mengine lakini fuatilieni nipate taarifa Jumapili narudi kwa ghafla tu kuja kuona taarifa ya takwimu aliyoitoa Mheshimiwa Waziri kama ni sahihi na hizo mlizopokea.

Kwa hili ni kwamba anapanga utaratibu wa kukaa na wananchi kila Jumatano, kuonana na wananchi moja kwa moja hasa katika asilimia 95 ya hoja zinazoletwa kwa Wakuu wa Wilaya hao ni ardhi, ni za ardhi, migogoro ya ardhi. Nilidhani Sheria ya mwaka 1999 itakuwa imeleta ufumbuzi, kumbe hapana bado matatizo yanajitokeza kuhusu ardhi.

Sasa hapa huenda vyombo vinavyotoa maamuzi vinakuwa na kigugumizi au (b) huenda Sheria yenyewe ilikuwa na tafsiri tofauti ambayo watu wanatafsiri vibaya. Kwa sababu afadhali kuelewa kitu kuliko kutokuelewa halafu ukatekeleza. Na hii ni hatari zaidi ukiielewa vibaya. Aliyeelewa hutekeleza, asiyeelewa hutekeleza visivyo. Aliyeelewa vibaya hutekeleza visivyo. Kwa sababu yako matatizo mengi yamejitokeza, sipendi kutaja neno mengi. Kwa sababu mengi siyo 1,000 pengine inatakiwa 900.

Na kidogo si moja pengine inatakiwa nusu. Kwa sikuweza kutumia neno hilo kwa usahihi wa Sheria ambazo zimeletwa. Kwa hiyo, suala la ardhi liangaliwe katika hali yoyote ya Sheria na utekelezaji na maamuzi ambayo yanafanyika na vyombo vilivyoyasimamia mambo haya ya ardhi, *otherwise* tumalize migogoro hii ya ardhi, tupewe *time frame* tupewe kwa mfano kabla ya mwaka 2005 tunaweza tukamudu matatizo madogo madogo ya wafugaji na hii inatokana kwamba badala ya kutumia samaki, baadhi ya watu binafsi katika vijiji wanauza ardhi yao wanachukua heka 200 wanampa mtu kutoka Dar es Salaaam, toka wapi, wanatoa pale.

Kwa hiyo, hati zile ambazo kama kuna ardhi katika vijiji Tanzania nzima, ambayo imeuzwa na mtu binafsi Kamati zilizotajwa katika Sheria ambazo hazijathibitishwa basi hati hizo ni batili, vifutwe na kama Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi itakuja hapa na hoja yake basi nitatoa *data* za baadhi ya vijiji ambavyo imeuza ardhi, wengine wanasema ni ardhi yao. Hakuna ardhi ya mtu. Kwa hiyo, kama imeuzwa kijijini wanafuata Sheria, kuna Hati za Miliki za kimila. Hapa napenda nipongeze kijiji cha Magila ambao wamekaa kama Serikali na kama wanavijiji kwa kukabidhi shamba ya mfanyabiashara mmoja. Huo ndiyo utaratibu mzuri, uwe mfano wa kuigwa kwa vijiji vingine, ardhi siyo mali ambayo inahamashika wala siyo mali inayoongezeka.

Watanzania tunaongezeka, tutahitaji ardhi hapo baadaye. Kwa hiyo, tusiwe tunajilimbikizia matatizo tukawa na Serikali bomu baadaye. Kwa hiyo, naomba Sheria ya Ardhi na Utekelezaji wa Ardhi waende sambamba kutatua matatizo badala ya kuongeza tatizo katika masuala mbalimbali.

Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, marekebisho katika Sheria ya Ardhi ambapo inapendekezwa wawekezaji watoke nje na mashirika na balozi zilizoko nchini kumilikishwa ardhi.

Hii ni hatari kwani tutajikuta nchi imemegwa na kupewa wageni ambao mara nyingi hunyanyasa wazalendo kwa kuweka mabango ya *no trespassing, private road, no entry* na kadhalika. Pia tutashuhudia bendera za nchi wanakotoka wawekezaji zikipepea kila kona. Hii ni kudhalilisha uhuru wa nchi yetu.

Uhusiano wa kibalozi si kitu cha kudumu na pale mahusiano yanapokuwa mabaya, balozi zinaweza kufukuzwa nchini. Si vema kumilikisha ardhi kwa wageni kwani pale mahusiano yakiwa mabaya yataathiri kurudishwa kwa ardhi hiyo Serikalini. Pia taasisi za nje na wawekezaji huchukua ardhi kubwa kwa matarajio ya kuitumia ingawa baadaye haiwi hivyo. Hii itapelekea kuwa na *speculation* tu na wala si uwekezaji.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru mara ya pili kwa kunipatia nafasi asubuhi hii niweze kuhitimisha hoja yangu kwa kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii. Lakini kabla ya kufanya hivyo na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kumpongeza kwa dhati sana ndugu yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wake alioupata katika Jimbo la Uchaguzi la Bariadi Mashariki. Namtakia kila la kheri katika jukumu lake jipya na kwa kurejea humu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kusema humu Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge wanane. Ningelipenda niwatambue tu kama taratibu zetu zilivyo. Nianze na

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira na mwisho kwa kutaja lakini siyo kwa umuhimu Mheshimiwa Semindu K. Pawa. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge wawili nao ni Mheshimiwa Beatus R. Magayane na Mheshimiwa Estherina Kilasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge. Mengi *of course* wametoa kama tahadhari, tuwe makini. Lakini mingine ni michango mizuri pia mapendekezo yaliyo mahususi.

Nianze na hili la jukumu jipya ambalo Serikali kupitia Muswada huu inapendekeza Sumatra iongezewe. Nalo hili la *research* na *rescue operations,* uokoaji. Hoja ilitolewa hata kwenye Kamati imerudiwa katika Taarifa. Ni kwamba Serikali ihakikishe kabisa kwamba inajenga uwezo kwa chombo hiki kwa sababu jukumu hilo ni jukumu muhimu sana na kama tulivyoeleza kwenye Kamati.

Napenda tu nirudie kwamba ni kusudio kabisa la Serikali kukiwezesha chombo hiki kiweze kutekeleza majukumu yake kama huwezi kukipatia nyenzo za kufanyia kazi maana yake ni kwamba lazima ukiwezeshe pia kiweze kukodi vyombo hivi kwa wale ambavyo wanavyo.

Lakini katika kujenga uwezo ndiyo maana tunapendekeza Mheshimiwa Spika, kwamba tukubali basi kuainisha kama miongoni mwa vyanzo vya mapato, gharama zile ada za ukaguzi wa meli unaofanyika kwamba waweze ku-*retain* uwezo wa kujiwezesha na tunasema pia kwamba kwa sababu sasa hivi tunajua tuna vyombo vyetu vya hapa ndani kwa upande wa wapiganaji, Jeshi la Wananchi wa Tanzania tunajua wakati wa matatizo ndiyo limekuwa mstari wa mbele sana katika kufanya kazi hii ya uokoaji na pia Jeshi la Polisi na pia Idara ya Zima Moto.

Sasa tunataka tuwe na chombo cha kuratibu shughuli hizi. Ndiyo maana Serikali inaweka uzito wa kipekee wa kuhakikisha kwamba maandalizi ya chombo hiki yanafanyika kwa makini na pia kipewe majukumu ambayo kweli yatakiwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi. Kwa hilo mimi naamini Serikali na nyinyi tuko pamoja kabisa hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, liliulizwa swali na Mheshimiwa Abdallah, udhibiti wa meli zinazoingia katika Bandari zetu. Je, meli za hapa nchini zitasimamiwa na nani? Ni kusudio la Serikali, ni hoja nzuri, lakini usimamizi wa meli ambazo zimesajiliwa ndani ni chombo hiki hiki. Lakini tunapenda tulifafanue vizuri ili kuondoa hii dhana ambayo imemsumbua Mheshimiwa Abdallah, kwa idhini yako Mheshimiwa Spika, kipindi tutakapoingia kwenye Kamati nadhani tutapendekeza, tutafanya marekebisho kidogo tu ili kulijibu kwa uwazi zaidi hoja ambayo Mheshimiwa Abdallah imemsumbua. Lakini kwa wazi, meli hizo zinadhibitiwa na chombo hiki.

Limekuwepo tatizo la uwelewa. Namshukuru sana Mheshimiwa Shellukindo kwa kueleza hili kwamba kwenye ibara hiyo ya 48, A Sumatra. Utaratibu wa katika Kamati ya mali za Sumatra. Lengo siyo kuwanyima watu haki na wala utaratibu huu haupingani na Sheria zingine wala Katiba, hapana. Ni utaratibu tu kwa vyombo vya Serikali kwamba Serikali imejiwekea utaratibu kwa sababu ni Serikali ina mali ambazo mali zake ni kwa niaba ya wananchi. Sasa inaweka utaratibu, wewe ukipata haki, ukipata haki yako dhidi ya Serikali, lakini unapotaka kutekeleza hiyo sasa haki umewekewa utaratibu wa kufuata na Serikali zote duniani huo ndiyo utaratibu. Huwezi ukafanya kamata kamata tu.

Mheshimiwa Spika, la msingi hapa linalosema katika Muswada huu ni kwamba mtu aliyepata hukumu dhidi ya chombo hiki ahakikishiwe analipwa na vyombo hivi ni vya Serikali, Serikali kama ilivyo Serikali ya Tanzania na Serikali zote, ni Serikali za kiungwana hizi. Unapopata uamuzi halali wa Mahakama isipokuwa pale uamuzi unapopingwa kwa njia ya rufaa ni vizuri ukaheshimu uamuzi huo kama ni kulipa, lipa.

Na ndiyo maana tunapendekeza kwamba chombo hicho kitatenga fedha za kuweza kulipa hukumu ambayo imetolewa dhidi ya chombo hicho lakini siyo kufanya kamata kamata hata pale ambapo wadaiwa wanaandika cheki kumlipa, unasikia gari imekamatwa, lori limekamatwa, boti imekamatwa. Sasa hiyo itakuwa ni vurugu na ndiyo maana tunataka tuweke utaratibu ambao ni mwananana, utaratibu ambao unatambua chombo hiki kina majukumu, utaratibu ambao unatambua pia kwamba chombo hiki inapostahili tuipe fedha kutokana na hukumu zilizotolewa.

Ilitolewa hoja pia kwamba Mheshimiwa Spika, kwamba kwenye ukurasa wa 32 wa Muswada kama ulivyochapishwa, kwenye ibara ya (g), kinasema *by adding immediatly after Section 48(b) as added the following,* unakuta *part 10* ndiyo inayofuata.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni tatizo la uandishi kwa sababu suala hili ni *technical* tu. Mngelikuwa nayo hiyo Sheria ya *SUMATRA* yenyewe mtaona kwamba tulifanya marekebisho kwenye eneo unapofika kwenye kifungu cha 48. Tumesema *Consequential transitional and miscelleneous provisions* hizo. Sasa ukiingalia kwa makini *transition* inahusu kifungu cha 48. *Consequential provisions* zinahusu marekebisho ya sheria zilizotajwa na Sheria ya *SUMATRA* yanayoanza baada ya kifungu cha 48 na ndiyo maana wanakuambia *by adding immediately after Section (b) as added the following,* sasa ndiyo unaanzisha sehemu mpya ya 10. Sasa hivi haya ambayo yapo katika kifungu cha 48 yako katika sehemu ya 9. Tunataka sasa consequential amendments ionekane wazi, kwa sababu vivuko, Sheria ya Vivuko, Sheria ya *TRC,* Sheria ya Mamlaka ya Bandari, hizi sasa ndiyo consequential kwa sababu tumefanya marekebisho kutambua ujio wa Sumatra kama chombo cha udhibiti kwa shughuli zilizotajwa katika maeneo hayo.

Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Spika, hayo maneno hayakuandikwa ili kuruhusu Serikali kuingiza vitu vingine kama inavyodaiwa, hapana. Ni waandishi tu wa Sheria iwe wazi zaidi, kilichokusudiwa kama consequential na kipi kilikuwa transitional.

Ushauri umetolewa, Sheria hata kabla wino haujakauka kwenye karatasi, marekebisho yanakuja Bungeni. Ni ushauri mzuri. Napenda tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kama nilivyomsikia Mheshimiwa Shellukindo kaka yangu. Ndiyo ukweli huo kwamba unapotaka kufanya maandalizi, fanya maandalizi mazuri, usione soo. *(Kicheko)*

Katika kuhakikisha kwamba ili sheria hii ianze vizuri kile ambacho sikukiona nimekiona sasa. Ni vizuri nikakisahihisha mapema na ndiyo maana tumekuja na hilo na vile vile Bunge lako Tukufu nilifahamishe tu kwamba Sheria inayosimamia tafsiri ya Sheria zote nchini inaruhusu kabisa kabisa kwamba Sheria ambayo haijaanza kutumika inaweza ikarekebishwa kwa utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, siyo kitu kigeni hicho, ni utaratibu ambao upo. Lakini hoja ya Mheshimiwa Shekiffu na wengine ninavyoelewa ni kwamba jamani nyinyi watu wa Serikali muwe mnatusaidia. Lakini na sisi Wabunge, maana zinakuja Bungeni na sisi tusaidiane basi. Ndiyo maana mimi sina tatizo na hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafao ya hawa watumishi wa chombo cha *Tanzania Central Freight Bureau* ambao hawatabahatika kuhamishiwa ajira yao Sumatra na wale ambao hawatahamishiwa katika Idara zingine za Serikali, rai ya Waheshimiwa Wabunge hapa ni kwamba jamani, wametumikia, wamefanya kazi nzuri, wametumikia chombo hiki kwa uaminifu. *(Makofi)*

Hii ya leo njoo, kesho njoo, isiwepo, walipwe mafao. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba halipo tatizo kwa upande wa mafao ya hawa ndugu zetu ambao ajira yao haitaendelezwa kupitia vyombo vingine vya Serikali. Serikali ililiona mapema sana na hata Bodi ya chombo hiki cha *Central Freight Bureau* imekuwa makini sana tangu mwanzo, wao michango wako *very current* michango yao ya uzeeni kwa mfuko wa *Pension* wa Mashirika ya Umma, wako *current* kabisa hakuna wasiwasi.

Lakini zuri Bodi ya *TCFB* kwa idhini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, iliunda mfuko maalum kabisa wa mafao ya wafanyakazi kwa ajili ya malipo ya kisheria na malipo ya ahsante yaani mkono wa kwa kheri. Kwa hiyo, liko *taken care of* na wasiwe na wasiwasi kwamba watapata matatizo katika haki zao. *(Makofi)*

Niseme kwa wale ambao ajira yao, Mheshimiwa Kilasi aliuliza kwamba ajira yao itahamishiwa Sumatra, je na wenyewe watalipwa kabla ya kuanza ajira mpya. Hapana, tunachosema ni kwamba ajira yao iendelezwe, manufaa yao kwa kipindi cha nyuma yatahifadhiwa na yachukuliwe. Lakini hawatalipwa siku ambayo wanaanza utumishi mpya. Muswada unapendekeza kwamba wasilipwe mishahara kule Sumatra wasipewe masharti ya kazi ambayo ni duni ya yale ambayo wanayapata sasa hivi lakini wanaweza wakapewa yaliyo bora zaidi. *(Makofi)*

Masuala ya Muundo wa Bodi ya Mkonge, Chai, nakushukuru sana Mheshimiwa Spika ulipotukumbusha tusome Muswada huu na hayo marekebisho. Inawezekana baadhi ya waliochangia hawakuwa wamefikia katika eneo hilo la marekebisho. Lakini Mheshimiwa Mwandoro alitumia maneno niliyotumia. Bodi hizi zimewekwa mikononi mwa wenyewe. Ilikuwa ni katika lile kundi la tatu la hawa Wajumbe wa Bodi hizi. Unaona kabisa kwamba kulikuwa na tafsiri kwamba kwa sababu kuna hawa wadau whether ni wakulima wadogo wa mkonge au association ya walimaji wa mkonge au hawa walimaji wadogo wa chai, inasema tu kwamba watatokana na huko.

Je, hoja hapa Mheshimiwa Spika, ni kwamba wadau hawa wanapokutana Dodoma au Lushoto au Muheza wanasema hawa ndiyo tumewateua. Wao wanateua au wanapendekeza. Sasa ilivyokaa, wao wanaweza kusema hakuna haja ya wewe Waziri kuteua sisi, sisi tunakuja tu kwa sababu tumetoka kwa wadau. Sasa tunasema tuinyoshe, mamlaka ya uteuzi iwe wazi.

Wadau wale taasisi zao zinatumika tu kuwapata, yaani wanapendekeza na ndiyo maana tunasema Waziri usimletee jina moja, utakuwa umeshamchagulia. Ndiyo maana tunasema wasipungue idadi hii nasema wasizidi hawa. Sasa leteni nyinyi mnapokutana huko, ndiyo Waziri atasema ah wote hawa wana sifa, basi mimi namchukua huyu. Mnataka wawili, Sheria inasema wawili, ninawachukua wawili. Ndiyo maana yake. Hakuna kiroja ambacho kinaletwa na hayo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Marmo aliyoyasema na sisi Serikalini tumeyafahamu. Sasa hivi ziko kesi nyingi sana zinazosubiri maamuzi ya migogoro ya ardhi nchi nzima na tunavyoifahamu Sheria hii unaanzia kijijini pale ndiyo ngazi ya kwanza halafu unakuja kwenye Kata ndiyo unakwenda kwenye Wilaya mpaka huko juu. Sasa limekuwepo tatizo, hilo la fedha mimi nadhani Mheshimiwa Marmo amelisemea vizuri na Serikali imesikia na sisi tungelipenda sana tuone *operationalisation* ya Mabaraza haya ya Kata, Vijiji mpaka juu kweli yanafanya kazi.

Haiwezekani Sheria ya nchi ikatungwa ambayo ina shabaha nzuri tu na tunajua migogoro ipo, lakini haiwezi ikatekelezwa kwa sababu ya matatizo ya fedha. Fedha zipatikane basi. Mabaraza haya yalikusudia yafanye kazi na wananchi wasipate kero ya kugombania viwanja mpaka mnataka hata kutoana macho kwa sababu ya kutokujua muende wapi.

Kwanza nawashukuru sana wananchi katika maeneo ambayo migogoro ipo, wamekuwa wavumilivu sana mpaka sasa hivi. Na hilo ndilo tunaloomba waendelee na hilo ili tukamilishe. Nashukuru sana Kamati, kwa sababu tuliwaeleza kwa nini tunatumia Mkutano wa Bajeti ambao siyo kawaida sana.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Spika, umeturuhusu kwa sababu ni eneo hili ambalo tusipolishughulikia sasa itabidi tuje *October.* Sasa tukasema busara imetutuma tu kama Serikali, tuna migogoro hii, angalau yale ambayo yalikuwa yanaonekana kwamba yana mapungufu kama ya kuapa mbele ya *RC* tuyamalize basi. Nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mmeelewa.

Tunaushuru sana uongozi wa Idara ya Mahakama kwa sababu wameliona kwamba katika kipindi hiki cha mpito, tunao Mahakimu wenye uzoefu sana kwa masuala haya, wanasema tuwatumie na hii napenda niseme wazi kwamba ni Bunge hili hili lilishauri Serikali jamani Mahakimu wana kazi nyingi sana, mnawaongezea tena kazi nyingine.

Sasa kwa nini msitafute watu wengine ambao wana ujuzi huo na wapo. Sasa ndiyo maana tumekuja na sura hii ya kuruhusu kwa kuanzia sasa hivi Mahakimu wetu ambao watateuliwa kuwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba kwa ngazi ya Wilaya watusaidie na huku Serikali inajiandaa katika kupanua ajira kwa hawa wengine ambao sasa hawatakuwa Mahakimu lakini watakuwa na zile sifa ambazo zimetajwa na Sheria.

Kwa hilo Mheshimiwa Spika, kama litafanyika nadhani tutaona sasa migogoro hii ya ardhi itaanza kupata ufumbuzi kama ilivyokusudiwa. Kabla sijafika kwenye eneo kubwa la ardhi nisemee tu hili ambalo Mheshimiwa Shekiffu alisema kwa upande wa Sumatra haya majukumu ametoa yeye tahadhari. Nashukuru, wote tulisikia hapa.

Nia ya Serikali ilikuwa mzuri. Tulitaka tuone kwamba chombo hiki cha Sheria ya *Merchant Shipping* kwa sura ile ambayo ina zile *regulatory functions* hasa kwa upande *safety* kama nchi moja tuweze kuyakidhi hayo. Lakini nasema mashauriano kati ya Serikali zetu mbili haya ni ya kudumu.

Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati ana-*wind up* Muswada wa Sheria ya *Merchant Shipping* ilikuwa kwamba kwa utaratibu huu tunategemea sana Serikali ya Mapinduzi kwamba haya ambayo tunayafanya ambayo yatawezesha nchi yetu kwa vyombo hivi vya usafiri wa majini kweli na wenyewe waweze kuwa na busara, umuhimu, uharaka na ulazima wa kutunga sheria ambayo itafanana na haya ambayo Bunge limetunga kwa upande wa Tanzania Bara. Mimi nadhani aliyosema Mheshimiwa Shekiffu tunayaelewa katika utaratibu huo.

Sasa nimalizie Mheshimiwa Spika, kwa mchango mkubwa ambao umetolewa kuhusiana na marekebisho haya ya Sheria ya Ardhi. Kwanza niseme kupitia marekebisho haya nimesikia neno linatumiwa ku-*liberalize* kuifanya ardhi kuwa huria.

Sio shabaha. Mimi nadhani siyo shabaha hiyo. Shabaha ya marekebisho haya ni kwamba tukubali kama Serikali, Serikali tukubali kama Bunge, tukubali kama Watanzania kwamba katika juhudi za kupambana na umaskini, kupambana na maradhi, kupambana na yote haya, kuhakikisha wananchi wetu wanapata elimu.

Kuna wadau wengine ambao wanashirikiana na Serikali. Sasa Sheria ilivyokaa sasa hivi, kifungu cha 19 kinasema mgeni yoyote hatapata ardhi hapa, isipokuwa kupitia kwenye mlango wa *TIC,* sasa Sheria ya *TIC* ni kufanya biashara.

Sasa wengi hawa hawafanyi biashara, *not for profit organizations* na wote tunafahamu na wengine tunaishi nao vijijini huko. Wengine tunao nje tu hapa na wao wanasema sisi ili tuweze kuyafanya haya tunahitaji ardhi na sisi kama mtu mwingine tujisikie kwamba hiki tulichopewa ni chetu. Tunapendekeza sasa kwamba angalau mlango tufungue kidogo lakini kwa masharti yale yale ambayo yamo katika Sheria ya Ardhi.

Ndiyo maana tunasema Kifungu cha 47, 48, 49 ukivisoma vile ndiyo yale masharti ya kunyang'anya, yule mtu ambaye amekiuka masharti ambayo amepewa, amemilikishwa kwa masharti, umekiuka ardhi yako inaondoka. Ulipewa tu fursa ya kutumia, wewe siyo mwenye ardhi hiyo. Wewe umepewa haki tu ya kutumia kwa masharti. Sasa ndiyo maana mapendekezo yameandikwa kutambua hiyo kwamba tunairekebisha Sheria moja, lakini marekebisho haya yatasomwa kama sehemu ya Sheria Mama Ndio maana tunaonyesha tu kwamba vifungu vile ambavyo viko kwenye sheria vitatumika pia kwa wale ambao walipewa kwa kuamini kwamba wana nia njema, shabaha ambazo zimeainishwa katika Muswada huu waka-*abuse* ile *hospitality* waliyopewa na Serikali basi Serikali kupitia mamlaka inayohusika watafutiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda Waheshimiwa Wabunge tuelewe shabaha ya Serikali. Shabaha ya Serikali haina nia ya kusema kwamba sasa mlango uko wazi kwa kila *NGO* ya kutoa nje inakuja kumilikishwa ardhi, hapana.

Utaratibu ni huo huo wewe lazima ujieleze wewe ni nani, hivi kweli utatusaidia katika maeneo unayosema ya huduma za jamii, kweli unafanya shughuli hizo, elimu au kueneza dini tuone yote haya maana Katiba yako unayo tutaiona na Serikali ikiridhika utapewa lakini kama utatumia vibaya imani ambayo umepewa na Serikali, Serikali haitasita kukuambia ahsante sana tunakunyang'anya.

Mheshimiwa Spika, kwa Balozi za nchi za nje ambazo ziko Tanzania hapa kwa sababu tuna mahusiano na sisi tuna Balozi za Tanzania kule kwao tunaomba ardhi wanatupa kwa masharti na sisi ili tutekeleze majukumu yetu tunasema na wao wanapoomba ardhi wasiambiwe kwenda *TIC* maana wale hawafanyi biashara sisi ni wanachama katika Taasisi za Kimataifa.

Kuna taasisi moja ya Kimataifa inataka kujenga *headquarters* yake Dar es Salaam wamegota kwa sababu wanaambiwa sheria ilivyokaa, wanasema jamani sisi tunataka tujenge lakini mtuhakikishie kwamba tunapata Hati maana sio pesa zetu ni pesa za Jumuiya ya Kimataifa na ambayo na Tanzania ni mwanachama. Sasa tunasema kwa nini tujikwamishe kama nchi kuwa na Makao Makuu ya chombo cha Kimataifa nchini kwetu kwa sababu jengo lile hata wakiondoka hawataondoka nalo mgongoni litabaki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio maana tunasema tuweke utaratibu huu ambao utawezesha azma ya Serikali ya kuwakaribisha hawa ambao wanashirikiana na wadau wengine katika kupambana na umaskini lakini na hawa ambao ni wajibu wetu kama

Serikali kushirikiana nao na wenyewe waweze kupewa fursa ya kuwa na miliki ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fursa ambao mgeni amepewa unaanzia katika eneo ambalo wahusika wanafanya shughuli zao. Ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa mifano ambayo mmeitoa hapa kama kweli mnajua taasisi hiyo ilipewa ardhi hiyo na Serikali kwa madhumuni waliyoiombea na sasa wanaitumia kinyume kabisa kwa nini tusubiri mpaka tuje Bungeni? Serikali ipo, ninyi ndio watu wa kwanza kuwaambia *no,* mambo hayaendi vizuri unakiuka utaratibu ardhi hiyo hukuomba kwa matumizi hayo naamini ikifika kwa Waziri mwenye dhamana hiyo hatasita kabisa kulishughulikia.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuisaidie Serikali katika hili pale ambapo tunaamini kuna mapungufu yataweza kudhibitiwa mapema sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ardhi kubwa kuzidi mahitaji, aah, naamini wanapoomba unaweza kupata au usipate. Naamini Wizara ya Ardhi watakuwa makini akiomba eneo kubwa watamwambia unaomba eneo lote hilo kwa ajili ya kufanyia nini? Kwa vile utakuwa umetoa mapendekezo yako baada ya kipindi fulani kama Sheria ya Ardhi, vifungu vya 47, 48, 49 vinavyosema kama baada ya kipindi hicho ulichosema utayafanya hayo uliyoahidi kuyafanya hukuyafanya basi Serikali ina uwezo wa kusema *no,* eneo ulilopewa naona hulitumii kama ulivyoahidi sasa tunachukua sehemu ubakie na eneo ambalo liko ndani ya uwezo wako. Kama tumbo lako ni dogo basi using'ang'anie utavimbiwa waachie wengine ambao wanaweza kula zaidi yako.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru sana wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunipatia nafasi hii. Nimejitahidi kidogo kujibu hoja zao kama yapo ambayo hayakujibiwa tutajitahidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie katika hatua inayofuata ili tuweze kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpassa) Alikalia Kiti*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004, *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wetu una vifungu viwili tu kwa hiyo tunaendelea.

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004).*

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotatajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunitambua. Kama nilivyosema wakati nahitimisha hoja yangu, katika ukurasa wa 28 wa Muswada kama ulivyochapishwa napendekeza Ibara ndogo ya (h) inayohusu *"The Surface and Marine Transport Registry Authority"* tuifanyie marekebisho ili ieleweke wazi kabisa kwamba udhibiti pia kwa meli ambazo zimesajiliwa nchini unaangukia katika chombo hiki.

Mheshimiwa Nwebtejutu, napendekeza sasa isomeke: *"To exercise Port State control of all foreign ships and fleet State control of all Tanzanian registered ships".* Tukifanya marekebisho hayo tutakuwa tumejibu hoja ambayo ilitolewa na pia tunaliweka bayana kabisa suala hili kwamba udhibiti huu wa meli za nje ambazo zinaingia katika Bandari zetu lakini pia ambazo zimesajiliwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, umesema tu ni ukurasa wa 28, ni kifungu kipi ambacho unakirekebisha?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nimesema kifungu cha (h).

*(Ibara iliyotatajwa hapo juu ilipitishwa na Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004,**
***(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2004 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2004)* na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Hatua zote za kupitisha Muswada huu zimekamilika na kwa sababu hatuna shughuli nyingine ambayo imepangwa zaidi ya hii, kwa hiyo, naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 06.12 Mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano*
*Tarehe 9 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*